

TAARIFA YA HABARI ILIYO KUU SANA KATIKA HISTORIA



Na tuendeleo kusimama, kwa dakika chache tu, kwa maombi mafupi.

² Baba yetu wa Mbinguni, tunapokikaribia kiti Chako cha Kiungu cha rehema usiku wa leo, tunashukuru kwamba kuna kiti cha enzi cha rehema, kwa kuwa lingekuwa ni jambo la kuogofya sana kwetu kuja kwenye kiti cha enzi cha haki. Lakini Kristo amelipia haya yote, haki, kwa ajili yetu na ametupatanisha tena kwa Baba yetu, nasi tunakuja sasa katika rehema, tukikusihi Wewe sana ulithibitishe Neno Lako pamoja nasi usiku wa leo, kwa kukutana nasi, ambapo imeandikwa ya kwamba, “Walipo wawili watatu wamekusanyika kwa Jina Langu, nitakuwa katikati yao.” Sasa, tunashukuru kwa ajili ya ahadi hii, nasi tunajua ya kwamba Wewe hutimiza kila ahadi.

³ Nasi tunakuomba uwabariki wale walio katika Njia, kwamba utawatia moyo, wamejitolea usiku wa leo, wote, wapate kutoka, na katika usiku huu wenye mvua na mbaya, wenye upepo, inaonyesha heshima zao na upendo Kwako. Sasa, tunaomba ya kwamba utawabariki wale walio wagonjwa na wahitaji usiku wa leo, wapate kuponywa ugonjwa wowote walio nao, kwa Uwepo Wako. Wabariki wale wasiokujua Wewe usiku wa leo, wape baraka kuu sana hata watacupenda, nao wataielekeza mioyo yao Kwako kabla ya kuondoka kwenye jengo hili. Tujalie, Bwana.

⁴ Wabariki watumishi Wako, wahudumu Wako, wainjilisti Wako, wote walio humu mkutanoni, na kwingineko. Roho Mtakatifu na awe maishani mwetu, kusudi wengine wapate kuangalia na kuona kiu kuwa Naye. Tunaomba, katika Jina la Yesu. Amina.

⁵ Mnaweza kuketi. (Nitaziweka hizi chini kwa muda mfupi tu.) Katika somo la Maandiko, usiku wa leo, kwa kuwa tutaingia moja kwa moja kwenye ujumbe kwa sababu ya kuchelewa kidogo, linapatikana katika Injili ya Luka Mtakatifu, mlango wa 24 na kifungu cha 32:

Wakaambiana, Je, mioyo yetu haikuwaka ndani yetu, hapo alipokuwa akisema nasi njiani, na kutufunulia maandiko?

⁶ Basi ujumbe wangu usiku wa leo ni huu: *Taarifa Ya Habari Iliyo Kuu Kuliko Zote Katika Historia*. Na somo langu ni “Njoo, Amini, Na Uende.”

⁷ Ninastaajabia siku hizo arobaini kuu, za ajabu, tukufu ambazo Bwana wetu alikuwa duniani akiwatokea wanafunzi Wake na wengineo baada ya kufufuka Kwake. Nimesimama mara nyingi na kuwaza, “Vipi kama ningalikuwa kule!” Na chini ya matarajio hayo makubwa, jinsi ambavyo kila kona njiani huenda ukakutana Naye, uso kwa uso, Bwana Yesu aliyefufuka. Ingekuwa ni msisimko wa jinsi gani kukutana Naye na kujua ya kwamba Huyu alikuwa ni Yeye!

⁸ Lakini basi, kwenye wazo la pili la jambo hilo, baada ya kuwazia jinsi ingekuwa ni furaha kuu kukutana na Bwana kama jamaa hawa walivyofanya, Kleopa na rafiki yake wakienda zao Emau... Naye akaongea nao siku nzima, wala kamwe hawakumtambua. Halafu basi, usiku ule alipowakusanya pamoja, wakati wao... Yeye alifanya kana kwamba angewapita, awaache, wakaingia kwenye hoteli ndogo, ama mahali pa watalii, nao wakamshawishi asiende, na akae pamoja nao. Nao wakaendelea kumshawishi, mpaka hatimaye akaingia pamoja nao.

⁹ Siku nzima, bila kujua Yeye alikuwa ni Nani, na ndipo walipomwingiza nda-... , ama, ndani na kufunga milango, alifanya jambo lililokuwa, apate kuwafanya wajue kwamba ilikuwa ni Yeye. Na baada ya kuzungunza Naye siku nzima, kumsikia akihubiri kwa hiyo miaka mitatu aliyokuwa duniani, halafu baada ya kufufuka Kwake kumsikia akihubiri, wala hawakumtambua mpaka alipofanya jambo fulani kama tu alivyolifanya kabla ya kusulubiwa Kwake, ndipo wakajua ya kwamba Huyu alikuwa ni Yeye.

¹⁰ Na sasa, si ni ajabu kwamba inahitaji kitu fulani upande wa mambo ya kimbinguni kutufanya tuelewe ya kwamba ni Yeye, ambapo mafundisho, yenyewe, hayatafaulu? Yeye kamwe hakuliagiza Kanisa Lake, wakati huo, kwenda na kufundisha Neno, Yeye alisema, “Hubirini Injili,” ama dhihirisheni Injili. “Nayo Injili ilikuja si kwa neno tu, bali kwa nguvu, na madhihirisho ya Roho Mtakatifu,” alisema Paulo. Sasa, kwa hiyo kifungu kinachofuata kinasema, katika Marko 16, “Ishara hizi zitaambatana,” ama kufuatana na, “wale, hao waaminio.” Ndipo mnaona, kuthibitisha Neno kunahitaji liambatanishwe na ishara ya ufufuo, kumfanya Yesu ajulikane kwa watu.

¹¹ Kwa hiyo ulikuwa ni wakati mzuri sana, hizo siku arobaini zenye fahari. Jinsi ningelipenda kuwa huko! Lakini basi, nikiwazia tena, ya kwamba ingalinibidi kuwa mwaminio, kwa sababu Yeye hakuonekana kwa mtu yeyote ila Kanisa Lake teule. Yeye huonekana tu kwa waaminio. Na kama alivyokuwa wakati huo, Yeye hawezi kubadilika, siku hizi Yeye angali anaonekana tu kwa Kanisa Lake teule, waaminio.

¹² Sasa, tunaona ya kwamba kulikuwa na wengi waliofundisha juu ya Masihi katika siku hizo, na kulikuwa na wengi

waliomtazamia Masihi ajaye, bali Yeye alikuwa na Kanisa lililoteuliwa, vivyo hivyo analo usiku wa leo. Na hapo ndipo, mahali nilipoachia jana jioni, Kanisa teule, na ndipo akaonekana kwa Kanisa Lake teule pekee, hao wengine hawakumtambua. Na kama angalikuwa hapa leo, angefanya tu vile vile alivyofanya wakati huo, aonekane kwa mwaminio aliyeteuliwa, Yeye kamwe haonekani kwa asiyeamini.

¹³ Kwa nini Yesu, baada ya kufufuka Kwake, kama Yeye alivutiwa sana na kila mtu kujua ya kwamba alikuwa amefufuka katika wafu, basi nashangaa ni kwa nini hakwenda kwa, vema, tuseme, Pilato, ama kwa Herode, na kuwaambia, “Mnaona, Mimi hapa. Mlidhani mliniweza, sivyo? Lakini niliwaambia nitafufuka siku ya tatu, kwa hiyo mimi huyu hapa?”

¹⁴ Ama kwa nini hakwenda kwa Kayafa, kuhani mkuu, ama kwenda kwenye kanisa la kiothodoksi, huko chini kwenye sinagogi, na kuwaambia, “Sasa, nyote daima mmeamini ya kwamba Masihi atakuja, naye Daudi alisema ya kwamba Nafsi Yake haitaachwa kuzimuni, wala hangemwacha Mtakatifu Wake aone uharibifu, kwa hiyo Mimi niko hapa, Yule ambaye mlimtundika msalabani, niko hapa katika ufufuo kuwathibitishia ya kwamba Mimi ndiye Masihi?” Kwa nini hakufanya hivyo? Kwa sababu kama hawangeweza kumwamini Yeye alipokuwa hapa duniani Binafsi kabla ya kusulubiwa Kwake, hawangemwamini baadaye.

¹⁵ Na kwa hiyo basi wangesema, “Kuna jambo lingine lililotukia, hakuwa amekufa kabisa, ama wanafunzi wake walikuwa na namna fulani ya kitu cha kuhifadhi maiti ambacho kilimfufua, ama jambo fulani lililokuwa limetukia.” Kwa hiyo Yeye aliwatokea tu wale waliomwamini, na kumpenda, na walioteuliwa kumwona. Hivyo ndivyo angefanya leo hii, kama angekuja leo, na ambalo amekuja, katika mfano wa Roho.

¹⁶ Nanyi mnaona ya kwamba Yeye hujionyesha tu Mwenyewe, kama tulipoachia jana usiku katika Ibrahimu, Yeye kamwe hakushuka kwenye kundi la Lutu, bali alilitokea Kundi teule, akaelekeza mgongo Wake kwenye hema, na kusema, “Yu wapi mkeo, Sara?”

¹⁷ Akasema, “Hemani.” Naye akawaambia yale yatakayotukia na—na jinsi walivyokuwa wanaenda kumpata mtoto huyu, naye Sara akacheka, Naye akasema, “Kwa nini Sara akacheka?” Naye Sara akajaribu kukanusha hilo.

¹⁸ Naye Yesu, wakati, Yeye alisema, “Kama ilivyokuwa katika siku za—za Lutu, ndivyo itakavyokuwa katika kuja kwake Mwana wa Adamu.” Mnaona? Sasa, Malaika huyo kamwe hakushuka kwenda kwenye kundi hilo la Sodoma, Yeye alikaa tu na Walioitwa watoke na Wateule. Hao walikuwa na wajumbe wao, nayo macho yao yalipofushwa wasiuone Mlango, bali lile Kundi teule lilimwona Mungu akidhihirishwa katika mwili.

¹⁹ Na hili, kwenye asubuhi hii kuu ya ufufuo, walimwona Mungu akidhihirishwa katika mwili. Mauti hayangeweza kumshikilia. Naye alikuja tu kwa Wateule Wake, si kwa makanisa hayo mengine hata kidogo, kwa Mteule Wake tu. Sasa, kwa nini hakuenda kanisani? Alifanya hivyo alipokuja, alikuja kwa walio Wake, wala hawakumpokea.

²⁰ Sasa Yeye amekuja katika mfano wa Roho Mtakatifu, katika ninii...si kwa kanisa, bali kwa Kanisa teule, nasi, Kanisa, tunapaswa kumpeleka kwa wasioamini. Sisi ndio tunaopaswa kuufanya Uzima Wake uangaze kupitia kwetu kusudi wengine wapate kuamini. Ni sisi, Kristo ndani ya Kanisa, tunaoungazia Uwepo Wake, unamfanya aonekane kwa wote. Kwa hiyo basi, Yeye, wakati anapojiangazia Mwenyewe mbele, kuendelea, hasa, kupitia maisha ya waaminio Wake walioteuliwa, wale walioteuliwa kwa ajili ya Uzima wa Milele, humpokea, Yeye alisema, “Kondoo Wangu huisikia Sauti Yangu, mgeni hawatamfuata, bali kondoo Wangu huisikia Sauti Yangu,” Alijidhihirisha Mwenyewe kwa Kanisa Lake lililoitwa na lililoteuliwa. Yeye hufanya jambo lile lile kwa Kanisa leo hii kujidhihirisha Mwenyewe kupitia viumbe Vyake, sisi, Kanisa, Kanisa lililoitwa litoke.

²¹ Ujumbe wetu, kwa hivyo, kwa kweli ndio taarifa ya habari iliyo kuu kuliko zote ambayo historia imewahi kujua. Kumekuwako na kila namna za imani za kujisingizia, na kadhalika, lakini ujumbe kanisa lilio nao ndio taarifa ya habari iliyo kuu kuliko zote iliyowahi kuufikia ulimwengu. Naam, bwana. Tulimzika, amekufa, bali amefufuka na yu hai tena. Alikuwa amekufa tulipomzika, na sasa Yeye yu hai milele. Ni mambo ya hakika kweli. Yeye hajafa, bali yu hai milele. Ni ujumbe wa jinsi gani, ni taarifa ya jinsi gani! Kanisa linapaswa kusisimkwa sana. Kanisa linapaswa kuwa likiwasha hii ndani ya mioyo ya kila mtu wanayekutana naye, Yeye hajafa bali yu hai.

²² Inapaswa kuwa vichwa vya habari kila mahali. Lakini hawaamini jambo hilo, hiyo ndiyo sababu haifanyi vichwa vya habari. Lakini kwa mwaminio, inafanya kichwa cha habari moyoni mwa mwaminio. Wakati anapoiona na kuitambua, inamsisimua zaidi ya kila kitu ambacho kingeweza kufanywa. Inatupa kichwa cha habari kinachoangamiza kitu chochote kile cha ulimwengu. Mara wanapoona Yeye yu hai na pamoja na Kanisa Lake, ni msisimko jinsi gani kwa mwaminio! Vichwa vikuu kuliko vyote vya habari ambavyo vingeweza kuandikwa, ni kweli, ujumbe wetu leo hii, ujumbe wa Pasaka.

²³ Lakini tunaruhusu Pasaka iwe siku moja katika mwaka, hiyo ndiyo Pasaka yetu, siku moja katika mwaka ni Pasaka. *Kila* siku katika mwaka ni, inapaswa kuwa Pasaka. Kila siku inapaswa kuwa siku ya msisimko ya ufufuo. Lakini mnajua nini, wameuchanganya ujumbe wa Pasaka, nao wameuchanganya na mayai ya rangi, na—na mashada ya kifua, na kofia mpya,

na sungura, na kwa hiyo Pasaka ni propaganda tu. Lakini kwa mwaminio anayejua, siku baada ya siku, wanaishi katika Pasaka, kwa sababu Yeye amefufuka katika wafu, Naye yu hai milele mioyoni, akijitambulisha Mwenyewe kwa Kanisa Lake, siku baada ya siku, “Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio.”

²⁴ Sasa, kama ukisema wewe ni mwaminio, na ishara hizo hazifuatani nawe, basi ama umesema jambo baya, ama unasema ya kwamba Yeye alisema jambo baya. Kwa kuwa Yesu alisema, “Ishara hizi zitafuatana na mwaminio, katika Jina Langu watatoa pepo, watasema kwa lugha mpya. Kama wangelikuwa wametiwa sumu, wakanywa kitu cha kufisha, hakingewadhuru. Wakiweka mikono juu ya wagonjwa, watapata afya.” Ishara za aina hiyo hufuatana na mwaminio. Na hao ndio Yeye huwatokea, kwa mwaminio, kwa hiyo basi hizo ishara hufuatana na mwaminio.

²⁵ Loo, ni jambo tukufu jinsi gani kwa Kanisa Lake, baada ya miaka elfu moja mia tisa, karibu miaka elfu mbili iliyopita, kujua ya kwamba Yeye yu hai! Tunakutana Naye kwenye kila kona ya barabara, kwenye kila kona, kila mahali tuendapo tunamwona Yesu, kuona Uwepo Wake ulio hai ukitiririka kama Nuru angavu kutoka kwa Kanisa Lake tukufu la Mungu aliye hai. Jinsi tunavyopaswa kuwa na shukrani kwa ajili ya jambo hilo!

²⁶ Huo ujumbe ulitolewa kaburini, “Njoni, mwone. Nendeni, mkawaambie.” Jambo la kwanza, “Njoo, na ushawishike.” Siku hizi watu hawataki kuja, kuona. Wale wanaokuja, hawawezi kuketi dakika kumi, dakika tano wakati mwingine, kama ukiwakera, wameondoka. “Njoo, uone.” Usichungulie tu ndani, simama ukachunguze.

²⁷ “Njoo, uone. Kisha, nenda, ukawaambie.” Hivyo ndivyo alivyowaambia wale wanawake asubuhi ile kaburini, “Njoni, mwone mahali *alipokuwa* amelazwa, lakini hayuko hapa tena. Kisha nendeni, mkawaambie wanafunzi Wake ya kwamba ‘Nitakutana nanyi huko Galilaya.’”

²⁸ Enendeni, mkawaambie akina nani? Wanafunzi wake waliochanganyikiwa. Hakika walikuwa wamechanganyikiwa, wala hawakujua la kufanya. Wengi wao walikuwa wamerudi kwenye nyavu zao za samaki, walitaka kurudia kuvua samaki. Walikuwa wamechanganyikiwa kwa sababu hawakujua nini, jinsi ya kupata riziki. Walikuwa wameamini kabisa ya kwamba Yeye alikuwa ndiye Masihi, Naye huyu hapa alikuwa amekufa, wa—wala hawakujua la kufanya sasa. Lakini, “Nendeni, mkaliambie kanisa hili lililochanganyikiwa kwamba mimi ni hai, nami nitawatangulia, nami nitakutana nao huko Galilaya, kama nilivyoahidi kufanya.”

²⁹ Kanisa hilo, lililochanganyikiwa wakati huo, si baya kuliko kanisa lilivyo siku hizi. Lingali limchanganyikiwa, haliwezi

kuyafahamu Maandiko, haliwezi kuelewa ni kwa nini Marko 16 iliandikwa katika Biblia, nao, wamechanganyikiwa sana, wanasema, “Haikuvuviwa.” Nao wanaona Maandiko mengine, na kusema, “Roho Mtakatifu alitumika wakati mwingine, wala sio siku hizi.” Wanaona Maandiko mengine ambapo miujiza ilikuwa ifanyike, nao wanadai ya kwamba siku zote za miujiza zimepita.

³⁰ Nena kuhusu kuchanganyikiwa! Wamechanganyikiwa zaidi sasa, kuliko walivyokuwa wakati huo, lakini kitu kama walivyokuwa, kwa sababu kitu pekee walichokuwa nacho hao wanafunzi cha kuwafaraji kilikuwa ni tukio lililopita. Nalo kanisa siku hizi zaidi sana liko hivyo, hata kwa Wapentekoste, wakijaribu kujiridhisha na Matendo 2:4, tukio fulani la wakati uliopita. Lakini, loo, ujumbe huo wa Mungu aliye hai ungali unaishi leo. Kwa nini mnafadhaika? “Ninaenda mbele yenu. Mimi sijafa, ni hai,” Yeye anasema, “milele.”

³¹ Lakini wenye fadhaa, walichanganyikiwa sana hata wanajaribu kuunda *itikadi* mpya, na haichukui muda mrefu mpaka *itikadi* hiyo mpya, ni kama sikuzote, inakuwa *itikadi iliyopitwa na wakati*. Wana mvua ya vuli, na mvua ya masika, na mvua ya kati, na *hii*, na *ile*, na *nyingineyo*, shirika la namna fulani, dhehebu, na inakuwaje kwalo? Linakufa, kama tu vile mashirika yote yanavyokufa.

³² Nao wa—wa—wanachanganyikiwa, “Vema sasa, hatujui la kufanya, hatuna budi kuwakusanya watu hawa pamoja. Ha—hatuna budi kujitenga na kundi *hili*, ama kutoka kwenye kundi *lile*.” Wangali wamechanganyikiwa tu, bila kujua la kufanya, hawajui ujumbe halisi wa Pasaka. Ujumbe halisi wa Pasaka haukuwa, kwenda kuunda madhehebu, ulikuwa, kwenda kuihubiri Injili, kudhihirisha nguvu za Roho Mtakatifu, na kumwacha Yeye alichukue Kanisa mkononi Mwake. Lakini wangali wamechanganyikiwa, hawajui la kufanya, na jinsi gani.

³³ Nao watu wanapaswa kutambua ya kwamba kila wakati, kote katika historia, ninamwomba mwanatheolojia yeyote, mwanahistoria yeyote, kuniambia kamwe, ambapo Mungu aliwahi kuchukua madhehebu na kufanya lolote mbali na kuunda kundi la watu. Ni mfumo wa kujibunia. Sio watu mle ndani, bali ni mfumo wa kimadhehebu. Na kila wakati ambapo Mungu alituma uamsho, Yeye alimchukua mtu fulani kutoka kwenye madhehebu fulani kuanzisha uamsho. Na kila wakati ambapo mtu huyo, wakati, baada ya kuanzisha uamsho, basi watu waliomfuata waliunda madhehebu, lilikufa papo hapo wala halikufufuka tena. Sasa, hebu nionyeshe ukurasa wa historia, na namba, ambapo dhehebu liliwahi kuinuka baada ya kuunda dhehebu, lilikufa papo hapo. Wanakuwa watoto waliozaliwa wakiwa wamekufa, nao ni watoto waliokufa. Wanachohitaji ni kutandikwa makalioni kwa Injili, hasa, kuwafanya Hai tena.

³⁴ Sasa, lakini kama ilivyokuwa wakati huo, wakati Wajumbe hawa walipotoka kaburini asubuhi ile, kuwaambia wanafunzi hawa kwamba alikuwa amefufuka katika wafu, na alikuwa hai miongoni mwao, na alikuwa anawatangulia, Naye angekutana nao mahali fulani, lingali ni jambo zuri jinsi gani, Kristo wetu angali anatutangulia! Kuna mwisho wa safari, “Nitakutana nanyi hewani asubuhi hiyo.” Nalo Kanisa, lingali linaamini jambo hilo.

³⁵ Kanisa halisi, la kweli la Mungu aliye hai, tunangojea badiliko hilo lije, tunapoangalia mwenendo wa Kanisa Lake, Uzao wa Ibrahimu, ukitokea jinsi alivyomfanyia Ibrahimu, nasi tungali tunangojea sasa mkutano huo mkuu hewani, ambapo tutamwona, tutanyakuliwa pamoja na wale ambao wamangojea nyuma yetu. Watafufuka katika wafu nasi tutahuishwa katika dakika moja, kufumba na kufumbua jicho, na kunyakuliwa kumlaki Yeye hewani, na kuwa pamoja na Yeye daima. Tungali tuna mwongozo, nasi tunapaswa kuushikilia huu, na kuuamini kwa mioyo yetu yote.

³⁶ Lakini wao, katika siku hiyo, walikuwa na shughuli nyingi kupita kiasi, walishughulikia mambo mengine, na kutupa nyavu zao, na kurudi kwenye uvuvi wao. Sisi leo ni vile vile, tumechukuliwa na mengi mbalimbali ya *haya*, *yale*, na *mengineyo*, na *itikadi* nyingi sana, na madhehebu mengi sana, na mashirika mengi sana, na mzee mkuu wa jimbo. Nasi hatuna budi kuwa waangalifu sana ni mkutano wa namna gani tunaoshirikiana nao, kwa sababu msimamizi wa wilaya atatufukuza. Na—na halafu kama tukishuka kwenda kwenye mkutano *fulani*, mchungaji atatufukuza. Na kama ninii, loo, askofu atatufanyia jambo fulani, ama kanisa litatutenga. Loo, nasi tuna shughuli nyingi sana kuwaangalia washiriki wetu tuone kwamba hawaendi kwenye kanisa lingine lolote, au kuwa na uhusiano wowote ila tu na kikundi chetu kidogo.

³⁷ Tunashughulika sana na hilo, ni kama tu kubadilishana washiriki, na ni kama tu kuhamisha maiti moja kutoka chumba kimoja cha maiti hadi kingine, kweli kabisa. Hawajui ufufuo umepita na tayari tunaufurahia, bali wanabadilisha maiti kutoka mahali pamoja hadi pengine, karibu tu jinsi inavyogeuka.

³⁸ Loo, ni vigumu kwao kulielewa, ya kwamba Kristo wetu yu hai, Yeye hajafa, bali yu hai milele, na Yeye ni yule yule jana, leo, na hata milele. Lakini tuna shughuli nyingi sana, tumechukuliwa na mambo mengi mbalimbali, kanisa lina mengi sana ya kufanya, na lina shughuli nyingi sana kuhusu *hili* na *lile*, hatuna wakati wa kuyachunguza mambo haya. Na kama tukisikia likitoka kwa mjumbe, “Loo, ni hadithi kama walizoamini wakati huo. Loo, hao wanawake wapumbavu walikuwa kule, ni vigumu kujua kile wao . . . Wanajiundia jambo fulani.” Mnaona, tuna shughuli nyingi sana na mambo mengine.

Kwa nini tusichukue muda kidogo kulichunguza? Tuketi mbele Zake, na, “Njoni, na tusemezane, asema Mungu. Ingawa kutokuamini kwenu ni kwekundu sana, kutakuwa kweupe kama theluji; ingawa ni kwekundu kama bendera, kutakuwa kweupe kama sufu.”

³⁹ Lakini tuna shughuli nyingi *sana*. Hatuna budi kuona ya kwamba hakuna mmoja wa uwili wetu anakuwa wa utatu, na wa utatu wetu hawi wa umoja, na kadhalika, inatubidi tu kuhakikisha ya kwamba tunaangalia jambo hilo. Na jambo ni kwamba, Kristo wakati wote anaishi katika Kanisa Lake, nasi tuna—tunaninii, kama nilivyosema, tunayabeba kutoka chumba kimoja cha maiti hadi kingine, na ndivyo hivyo. Sasa, hivyo ndivyo tu ilivyokuwa wakati huo, hivyo ndivyo ilivyo siku hizi, kitu kama hicho.

⁴⁰ Watu wengine huifanya Injili kuwa msafara wa mazishi. Hiyo ni kweli. Wanaenda kanisani kana kwamba tu ilikuwa msafara wa mazishi. Wengine wanaifanya burudani. Hiyo ni kweli. Baadhi yao wanaifanya tu burudani, wakati mzuri tu wa kwenda kucheza muziki chungu nzima, kurukaruka jukwaani, kucheza kila mahali jukwaani, ama chini kwenye marefu ya kanisa, na kukimbia, kuketi chini, na kuzungumza juu ya majirani zao. Hiyo ni kweli. Baadhi yao wanaowazia wanapaswa kusimama na kukariri doksolojia, na kanuni ya imani ya mtume, *wanavyoita*. Ninataka mninii, mtu fulani, anionyeshe jambo moja lililoandikwa Mle ndani ambalo ni kanuni ya imani ya mtume. “Ninaamini Kanisa Takatifu la Katoliki ya Kirumi.” Mimi siliamini. “Ninaamini katika ushirika wa watakatifu.” Huo ni uabudu mizimu, siuamini. Lakini wana shughuli nyingi sana wakijitungia mambo hayo, nao wanalifanya msafara wa mazishi.

⁴¹ Si msafara wa mazishi, na wala si burudani, ni karamu, karamu pamoja na Kristo, wakati waaminio:

“Njoo ule,” Bwana anaita, “Njoo ule;”
Unaweza kula mezani pa Yesu wakati wote;
Yeye aliyewalisha makutano, akayageuza maji
yakawa divai,

Yesu yuyo huyo yu hai usiku wa leo.

Kwa mwenye njaa anaita sasa, “Loo, njoo ule.”

Ni karamu na si—si mchezo, na wala si msafara wa mazishi.

⁴² Sasa, ule ujumbe ni kwamba Yeye anatutangulia, anatutangulia. Hayuko kaburini nyuma yetu, Yeye yuko mbele yetu, akitengeneza njia. Inatupasa kufuata, sio kuangalia nyuma kaburini, bali kuangalia mbele, jinsi Yeye anavyoongoza. Kwa kuwa Yeye ndiye Kiongozi wetu, tunapaswa kumfuata, sio kuangalia nyuma makaburini.

43 Mariamu, asubuhi hiyo, aliwakilisha vema kanisa lililochanganyikiwa. Aliliwakilisha vizuri, kwa sababu alikuwa katika m—mfereji ule ule linalokalia siku hizi. Alisema nini alipomsikia akisema, “Mariamu, nini . . . ? Mwanamke, kwa nini unalia?”

44 Akasema, “Wamemwondoa Bwana wangu, nami sijui wamemfanyia nini.” Hivyo karibu ndivyo kanisa linavyosimama siku hizi, “Walimwondoa Bwana wangu, nami sijui nitampata wapi. Nimejaribu ushirika wao wote, nimejaribu mabatizo yao yote ya maji, nimewajaribu Wamethodisti, Wabaptisti, Wapresbiteri, Wapentekoste, Wakatoliki, na wote, wala siwezi kumpata. Sema Maandiko yanasema Yeye ni yule yule jana, leo, na hata milele, Yeye yuko mahali fulani. Kama hajafa basi Yu hai, hawezi kuwa hai na amekufa wakati uo huo.” Kwa hiyo Mariamu aliliwakilisha kanisa vizuri, “Wamemwondoa Bwana wangu, wala sijui ni wapi . . . wamefanya nini Naye.”

45 Kanisa linawazia siku hizi, “Loo, kulikuwako na Kristo mashuhuri wa kihistoria. A—aliwaponya wagonjwa, angeweza kuyatambua mawazo ya moyo wao. Alikuwa ni Kristo wa kihistoria. Aliwajia makutano, akaja kwa Petro, na akamwambia Petro, jina lake aliitwa Simoni, kasema, ‘Jina lako ni Simoni, jina la baba yako lilikuwa ni Yona.’ Loo hakika, huyo aliyefanya hivyo alikuwa ni Yesu. Hiyo ilikuwa ndiyo ishara ya Masihi, kulingana na Maandiko, yale nabii aliyosema.”

46 Kamwe hakufundisha jambo moja, wala Paulo. Wakati Paulo alipoletwa mbele ya Agripa, alisema, “Nimehubiri tu yale ambayo Musa na manabii walisema yangetimia. Basi kwa nini mnihukumu,” akasema, “wakati nimesema tu yale aliyosema Musa, yale manabii waliyosema yangetimia? Je, ni neno lisilosadikika kwako, loo, Agripa, kuamini katika ufufuo wa wafu, nataka ujue ya kwamba Mungu ni ufufuo wa wafu?” Ndivyo alivyo siku hizi.

47 Sasa, lakini Mariamu alisema, “Vema, sisi . . . Ninajua wakati mmoja nilimjua Yeye.” Lakini alikuwa akilia kwa huzuni, kwa sababu wakati mmoja alimjua Yeye, lakini Yeye . . . walikuwa wameninii, walikuwa wamemwondoa. Na hivyo ndivyo ilivyo siku hizi. Kila mmoja wetu anajaribu kwa namna fulani ya theolojia ya kifalsafa kushindilia, pamoja na namna fulani ya saikolojia kooni mwa mtu fulani na kuwaambia, “Tu—tunaamini *hiki*, na tunaamini *kile*.” Lakini Yesu alisema, “Aniaminiye Mimi, kazi nizifanyazo Mimi, yeye naye atazifanya.”

48 Nalo kanisa likasema, “Wamemwondoa Bwana wangu.” Walimfanyia nini? Hata hivyo, siku hizi, wengi kwa sababu ya ukosefu, na uvivu, na kukonda kwa kanisa, wanaamini ile hadithi ya Kiyahudi, huko nyuma, iliyosimuliwa, kwamba

walikuja wakamwiba kaburini usiku, bado wanafikiri ni kweli. Ninaamini ilikuwa yapata asilimia sabini ya Waprotestanti hata hawakuamini katika u—ufufuo wa kimwili, ama kuja halisi, takwimu ilionyesha hilo. Wanaukana tu. Wengi wao, maelfu yao wanakana kule kuzaliwa na bikira.

⁴⁹ “Wamemwondoa Bwana wangu.” Kwa nini? Hawana budi kufanya hivyo. Kama huwezi kuamini katika ufufuo wa kimwili, basi huwezi kumhubiri Kristo ambaye ni yeye yule jana, leo, na hata milele. Huwezi kuliadini Neno Lake, basi vipi kuhusu hilo? Tunajifanya wenyewe wasioamini na makafiri. Si ajabu maskini kanisa hulia, “Yuko wapi Bwana wangu? Yuko wapi Mungu wa historia? Yuko wapi Yesu aliyekuwako, aliyesema atakuwa pamoja nasi, daima Yeye angetutangulia, Naye angekuwa ndani yetu hata ukamilifu wa dahari, kazi alizofanya?”

⁵⁰ Na wakati kanisa linapooni hilo likitimia, wanashikwa na shughuli nyingi sana katika kuunda madhehebu, na hilo halikutoka kwenye shirika lao, wanaliita ibilisi, na kulitupilia mbali, jinsi hasa walivyofanya wakati huo. Kwa hiyo bado ni kuchanganyikiwa!

⁵¹ “Wamemwondoa Bwana wangu. Nimeenda kwenye meza ya ushirika, wakaniambia kama nikija, nile ekaristi takatifu, na—na kuliadini kanisa ambalo. . . Vema, nilienda na nikafanya hivyo, nami niliona nini? Hamna kitu. Theolojia nyingi, saikolojia nyingi, lakini kumwona Bwana wangu aliyefufuka, sikumwona. Waliniambia kama ningenyunyiziwa, bila shaka ni—ningempata, nami nikafanya hivyo. Waliniambia kama ningebatizwa kifudifudi, hamna lingine, kinyumenyume, ningempata hivyo. Nimefanya mabatizo yote, nimejiunga na makanisa yote, nilisoma kanuni zao zote za imani, ila yuko wapi Bwana wangu? Ni nani aliyemwondoa?”

⁵² “Wamemwondoa.” Ni nani aliyemwondoa? Madhehebu yalimwondosha. Sasa, hebu kanusha hilo wakati mmoja, nami nitakuthibitishia ya kwamba hilo ni kulingana na historia hasa, kitu kilichomwondoa, kilichounda kanisa Katoliki, kilikuwa ni dhehebu. Nao Waprotestanti wanageuka moja kwa moja, na kufanya jambo lile lile kanisa Katoliki lililofanya, kuunda dhehebu kutoka kwake. Basi unapofanya hivyo, unamwondoa Mungu. Angalia historia, angalia Maandiko, uone kama hayajatimia, hasa. “Wamemwondoa.”

⁵³ Nina ndugu mmoja kule, yeye ni wa Umoja, tena nina mmoja hapa aliye wa Uwili, kisha nina mmoja hapa chini ni *kitu kingine*, ama kitu kama hicho. Ni kitu gani? Ni *itikadi* ndogondogo ambazo zinakuwa, baada ya kitambo kidogo, *itikadi zilizopitwa na wakati*. Hiyo ni kweli. Lakini ni kitu gani? Ujumbe ungali unabaki vile vile: Kristo alifufuka katika wafu. Usimwelekeze mtu kwenye dhehebu fulani, ama kwenye namna fulani ya kitu fulani, mwelekeze kwa Yesu Kristo, Ambaye ni

yeye yule jana, leo, na hata milele, Yeye amefufuka katika wafu, Naye Ndiye wa kuangaliwa. Siku hizi tunataka kuwaelekeza kwenye baadhi ya shule zetu kuu za theolojia, baadhi ya madhehebu yetu.

⁵⁴ Lakini uponyaji wake ulitokana na kulia kwake, na kufiwa kwake. Tiba yake ikaja, kukata tamaa kwake kulikwisha aliposikia jina lake likiitwa, ndipo akamtambua Yeye kama Bwana wake. Naye akaulizwa, “Kwa nini unamtafuta aliye hai miongoni mwa wafu?” Basi Mariamu akaona kwamba Bwana wake hakuwa katika kanuni hizo za imani zilizokufa. Na mara kanisa litakapotambua, kama Mariamu alivyotambua, ya kwamba Bwana wetu aliyefufuka hayuko katika kanuni ya imani, yuko katika tukio la kibinafsi la ubatizo wa Roho Mtakatifu ndani ya moyo wa mwaminio. . . Yeye hayuko katika kanuni ya imani, Yeye hayuko katika madhehebu ya kanisa, Yeye hayuko, Yeye yuko katika moyo wa mwaminio. Hakuwa pamoja na makaburi yao yaliyokufa, huko nje, bali alikuwa hai.

⁵⁵ Loo, ni—ni ujumbe wa jinsi gani wa kuupeleka kanisani usiku wa leo! Je, wanaupokea? Si zaidi ya, basi. . . mbaya sasa kuliko ilivyokuwa wakati huo. Wanafunzi waliposikia hayo, waliamini, nayo Biblia ilisema walifurahi. Biblia ilisema, “Waliposikia haya, walifurahi,” walipokutana Naye na kutambua ya kwamba huyo alikuwa Ndiye Bwana wao. Ndivyo ilivyo usiku wa leo, wakati mwanamume ama mwanamke, mvulana au msichana, ambaye yuko tayari kwenda nje ya kanuni ya imani ya kanisa lako. Sikuambii usiwe mfuasi wa kanisa lako, hiyo ni sawa, lakini kamwe usiifiche nafsi yako nyuma ya kanuni hiyo ya imani, ukifikiri hiyo itakuokoa. Kamwe hutaokolewa mpaka utakapompata Kristo kama Mwokozi wako binafsi na Roho Wake ayajaze maisha yako, ndipo ishara hizi zitafuatana na hao waaminio.

⁵⁶ Si dansi ya kuchezecheza, kama mlivyoona Wapentekoste wengi wakifanya, si nyumba ya kuhifadhia maiti, kama unavyowaona wengi wa hao wengine wakifanya, nao Wapentekoste karibu wametoka kwenye michezo yao sasa, wamerudi kwenye nyumba ya kuhifadhia maiti, pia. Si namna hiyo, huwatambulishi kwa jambo hilo, bali kwa Kristo aliyehai, aliyefufuka. Amina. Hilo ndilo tunalopaswa kuninii. . . Ndipo una furaha. Kama vile wale wanafunzi, unapokutana Naye, nawe unajua, na wakati alipofanya hiyo ishara mbele yao na kuwaonyesha ya kwamba Yeye alikuwa ni Yesu yeye yule, akifanya mambo yale yale aliyofanya, hakuna mtu mwingine angaliweza kuifanya hiyo ila Yeye, ndipo wakatambua ya kwamba Huyo alikuwa ni Bwana wao nao wakafurahi.

⁵⁷ Mbona, Theofilo na hao wengine, iliwachukua siku nzima kwenda Emau, safari ya siku ya Sabato moja, hawakuchukua ila dakika chache tu kurudi. Loo, baada ya wao kujua ukweli, kwamba Yeye alikuwa amefufuka, kwa sababu walikuwa

wamemwona Yeye akilihifadhi Neno Lake, na kulitimiza, na kufanya kama vile alivyofanya hasa kabla hajasulubiwa, walienda mbio kote nchini, nafikiri walikuwa tu wakikanyaga kila yadi nne ama tano. Walikuwa na haraka, walitaka kuwaambia hao wengine, “Kweli Bwana amefufuka kweli!” Walikuwa na kitu fulani moyoni mwao.

⁵⁸ Hawakuwa wakienda kule kubishania hoja zao za kidini, walikuwa wakienda huko kusema, “Ninajua Yeye yu hai. Ninamjua kwa sababu alitutokea, nasi tumemwona akifanya jambo lile lile alilofanya kabla hajafa, kabla hawajamwua kule juu. Wala kamwe hawakuiba mwili Wake, nao hao wanawake wanasema kweli kabisa, kwa sababu kweli Yeye alifufuka katika wafu, kwa sababu ilikuwa ni Yeye.”

⁵⁹ Ndipo wakaangaliana waliposimama chini ya, mahali fulani kupumzika kidogo, “*Hee, hee, hee.*” Kisha wakasema, “Je, mioyo yetu haikuwaka ndani yetu? *Hee, hee.* Tulipaswa kujua ya kwamba huyo alikuwa ni Yeye, jinsi alivyorejea huko nyuma kabisa katika Maandiko. Sisi...Je, mioyo yetu haikuwaka ndani yetu, hapo alipokuwa akisema nasi njiani, na kuyafungua Maandiko?”

⁶⁰ Kasema, “Enyi msiofahamu na,” Yeye hakuninii... “wenye moyo mzito kuelewa. Haikumpasa Kristo kuteswa, na kuingia katika utukufu Wake,” kama vile Maandiko yalivyosema.

⁶¹ Mnaona, walijua huyo alikuwa ni Yesu, kwa sababu Yeye aliambatana moja kwa moja na Maandiko haidhuru wengine walisema nini. Mara kanisa litakapofikia mahali litakapolingana na mafundisho ya Maandiko badala ya kujaribu kuchukua theolojia fulani ya kujibunia, ndipo mtakapompata Kristo aliyefufuka. Hiyo ni kweli, ndugu yangu. Mungu hajengi juu ya msingi mwingine ila ule uliowekwa tayari na mitume. Hiyo ni kweli. Loo! Naam, walifurahi.

⁶² Makanisa ya siku hizi yamebadilika yakawa kama yalivyokuwa kwenye Siku ya Pentekoste, hata hivyo. Loo, ni mabadiliko kiasi gani wamefanya tangu siku hiyo! Makanisa yanakutana siku hizi kuheshimu, inaonekana, nachukia kusema jambo hili, lakini inaonekana kwangu kana kwamba makanisa yanakutana siku hizi kuheshimu maiti. Wanaingia mahali hapo na kuimba *Karibu Zaidi, Na Wewe, Mungu Wangu*, na kitu fulani cha pole pole, *cha chumba cha kuhifadhi maiti* namna hiyo, kinatoa sauti ya uchovu. Mbona, wa—wanakuzunguka, wanasema, “Sasa, hebu sasa tukariri kanuni ya imani ya mtume. Hebu na turudie kanuni *fulani* hii ya imani ambayo Dk. *Nanii*, wa *ninii, nanii*...” Loo, jamani! Kama kwamba ulimsikitikia.

⁶³ Huku nusu yao wanakaa nyumbani kutazama televisheni, badala ya kuja kanisani Jumapili. Hiyo ni kweli. Wamekufa, ni—ni maiti tu inayozurura, halafu maiti ikihubiri, na maiti ikijaribu, kusimulia habari za maiti ambayo iliishi wakati

mmoja, na kuishi kaburini miaka mingi iliyopita, maiti. Na ni maiti, maiti, maiti tu!

⁶⁴ Wanaenda kumheshimu Kristo aliyekufa miaka elfu moja mia tisa iliyopita. Hapo karibu ndipo hasa mahali makanisa yalipo siku hizi, yakijaribu kuheshimu maiti, badala ya kumshangilia Mshindi. Amina. Utukufu kwa Mungu! Nina furaha kuwa Mpentekoste moyoni, si kwa madhehebu, la, bwana, kulifutilia mbali jina langu kutoka humo, bali kama tukio. Hatuji, hatumheshimu mtu fulani aliyekufa, tunamshangilia Mshindi, Yule aliyeshinda mauti, kuzimu, na kaburi, na magonjwa, kila pepo, kila kutokuamini, akakushinda.

⁶⁵ Sasa, unaweza kuwazia kama shule hii, hapa, ilikuwa na timu ya besiboli, ama timu ya mpira wa vikapu, nao wakatoka na kumshinda mshindani wao kisha wakarudi, ungeweza kuwawazia wakisisimama kama vile, wakiimba namna fulani ya maskini wimbo kama *Karibu Zaidi Na Wewe Mungu Wangu* kwao? Mbona wanazipeperusha bendera na kuwashangilia sana wakifanya... Vipi kuhusu wakati Napoleon aliporudi? Vipi kuhusu Stalin, wakati walipoenda Ujerumani, jinsi walivyofyatua bunduki na kufanya ninii ya Kijeruma... , ama, sa—saluti, na kuingama miguu yao kwa saluti hiyo ya Kirusi? Vipi kuhusu wakati wavulana wetu waliporudi nyumbani kutoka kwa ushindi wao? Filimbi zililia, watu wakaingia wazimu, wakapiga bunduki, wakapiga mayowe, wakapiga kengele. Kwa nini? Tulikuwa tumemshinda adui yetu. Utukufu!

⁶⁶ Na siku hizi ungefikiri uko kwenye namna fulani ya chumba cha kuhifadhia maiti, wanaingia kanisani nao, "*Tunamwamini Mungu Baba Mwenyezi.*" Ninaamini katika Yesu Kristo aliyefufuka, amina, Mshindi wa mauti, kuzimu, na kaburi. Ninaamini ya kwamba Yeye yu hai usiku wa leo, na katika jengo hili, yu hai, pamoja nasi kulingana na ahadi Yake, "Walipo wawili watatu wamekusanyika, nitakuwa katikati yao." Naam, bwana. Si ibada fulani ya mazishi, bali kumshangilia Mshindi Mwenye Nguvu!

⁶⁷ Lakini shida yetu, hatuungalii Mshindi wetu, tunamtazamia mzee wetu wa jimbo, tunamtazamia mwinjilisti fulani mashuhuri, mtu fulani wakati... tunaona wanayosema juu yake, naam, bwana. Tu—tu—tunatazamana, bali tumeamriwa kumwangukia Yeye. Tunatazamia kusema, sasa kama kuna *jambo lingine* linaloendelea, "Vema, Bwana alifanya jambo fulani, alimponya mtu fulani, alifanya jambo lingine kama hilo."

⁶⁸ Lakini, "Vema, sasa," tungenesema, "hebu tuone kile Dk. Jones asemacho juu yake. Endapo kanisa letu haliamini hilo, ha—hatutalipokea." Mnaona? Unaangalia yale mzee wa

jimbo asemayo, unaangalia yale askofu asemayo, basi kamwe hutamwona Kristo.

⁶⁹ Waliposikia ya kwamba Yesu alikuwa amefufuka katika wafu, na akaonekana miongoni mwao namna hiyo, hawakusimama na kuangaliana, walimwongalia Yeye. Waliona makovu Yake, waliona nguvu Zake, walimwona akifanya miujiza aliyofanya kabla hajafa, nao wakajua ilikuwa ni Mungu wao aliye hai, nao hawakuangaliana, wala hawakumwomba mtu yeyote awaangalie.

⁷⁰ Lakini leo hii, wenye kujigamba wanatokea, “Mimi ni Dk. *Nanii* mwenye elimu *fulani*. Mimi nina Ph.D., LL.D., Q.S.T.,” na mambo ya—ya namna hii nyingine yote, bali yuko wapi Kristo katika hayo yote? Tuna nini? Nyumba ya kuhifadhia maiti, na kumwabudu Kristo aliyekufa kaburini. Hatumwabudu Kristo aliyekufa kaburini, Kanisa lililo hai, Kanisa la Mungu aliye hai, tunamwabudu Mshindi aliyefufuka, ambaye alishinda kutokuamini kwetu, na kanuni hizo zote za imani, na kuwabwaga chini ya miguu Yake, na kusema, “Mimi ni wenu, nanyi ni Wangu.” Amina. “Mimi ni hai milele.” Huyo ndiye Mshindi Mkuu, Huyo Ndiye, Huyo Ndiye ambaye imani yangu inamwangalia.

⁷¹ Kile tunachotaka kufanya leo ni kutowaangalia hao maskini, wenye huzuni wanaokula vitunguu saumu huko nyuma, huko nyuma nyikani, wakitamani vyungu vya nyama vya Misri, waliokuwa wanavaa kaptura na mavazi na midomo iliyopakwa rangi, na kukata nywele zao, na kukana nguvu za Mungu, achana nao, wataangamia huko nyikani, hebu tumfuate Yoshua wetu mkuu, haleluya, Kiongozi wetu. Usiulize maswali yoyote, endelea tu kupiga hatua, hivyo tu. Endelea tu kusonga mbele. Usigeuke nyuma kuwaangalia, usiwajali hata kidogo. Wao wanataka kukaa Misri, na kuona kiu ya mambo ya ulimwengu na maskini mabingwa wao wote wa sinema na waigizaji na kadhalika, waache waendele. Tunamtazama Yesu, tunamtazama Yoshua wetu.

⁷² Hatuwatazamii wenye kiu. Shida yake ni kwamba siku hizi, mnasema, “Sasa, ngoja, hupaswi kunywa pombe, hupaswi kwenda kwenye sinema, hupaswi kufanya *hivi*, hupaswi... wanawake hawapaswi kukata nywele zao, hawapaswi kuvaa kaptura.” Loo, ninawazia kama mtu fulani amewahi kufika kwenye ile Nchi nyingine, na awahi kula baadhi ya zabibu kutoka Kanaani, kula baadhi ya makomamanga, na baadhi ya asali nzuri kule, hawataki kitunguu saumu tena cha ulimwengu.

⁷³ Jambo ni kwamba, tunawalisha tu maskini vitunguu saumu na kadhalika, na kuwaacha waone kiu na kuumwa na tumbo, samahani kwa tamshi hilo, hilo si sawa mi—mimbarani. Lakini rudini nyuma, kama wanataka kuuendea ulimwengu, waacheni warudi nyuma, sisi tunasonga mbele. Tuko katika... tutafuata

ninii yetu. . . Si kurudi tu kwenye Matendo 2:4, kutangatanga huko nyuma kwenye maeneo yale yale. Walifanya nini? Walikaa huko miaka arobaini, nao wakafia huko. Moja kwa moja huko nyuma juu ya maskini kitu kile kile, wakati wote. Hiyo ni sawa, Matendo 2:4 ni sehemu yake, lakini jambo ni kwamba, Yeye alisema, siku moja, kwa nani Wake. . . “Simama, umekuwa kwenye mlima huu kwa muda wa miaka arobaini, geukia kaskazini, vuka ng’ambo ya Yordani, ule utengano, kwa kuwa kuna zaidi ya mlima huu kwa ajili yenu.” Kuna zaidi ya Matendo 2:4 kwa ajili yenu, kila ahadi katika Kitabu hiki ni mali ya Kanisa, naye Mungu anangojea Kanisa Lake liinuke na kuipokea.

⁷⁴ Unawezaje kufanya hivyo wakati ungali una kiu na unataka kuwa kama ulimwengu? Wanawezaje kufanya hivyo wakati wangali wanakula, wanatamani kitunguu saumu, vyungu vya nyama vya Misri? La. Endelea kumfuata Yoshua. Hiyo ni kweli. Chukua zabibu mpya na Divai mpya ya Kipentekoste, ulewe Kwake, Ndugu, huta—huta—huta—hata hutautazama ulimwengu tena, *jambo fulani* litatukupata.

⁷⁵ Loo! Hebu na tusonge mbele tu, tukizifuata nyayo za Kiongozi wetu mkuu, na kuushinda. Kumbukeni, Mungu alimwambia Yoshua, “Kila mahali nyayo za miguu yako zitakapokanyaga, huo ni urithi.” Ndugu, basi nyayo zinamaanisha urithi. Hebu tuendeleo tu kutembea tuingie kwenye Nchi ya Ahadi, bila kuangalia nyuma kuona yaliyokuwa yametukia huko nyuma, na yale afanyayo mtu mwingine, weka macho yako kwa Yesu, yule Yoshua, yule Kiongozi. Endelea tu kusonga mbele, vina virefu zaidi na vimo vya juu zaidi, mpaka utakapomiliki kila kitu ambacho Mungu alikuahidi katika Neno Lake.

⁷⁶ Watu wote hawawezi kupokea hili. Jambo hili limefichwa macho ya ulimwengu, na ni upumbavu kwao, bali wale waliozaliwa na kuchaguliwa kwa ajili ya Uzima wa Milele, wanaliadini. Tunaona saa tunayoishi. Hebu na tusonge mbele, tukikumbuka jambo hili, kwamba tuna kitu Fulani nyuma yetu, Yesu alisema, wakati alipowatuma wanafunzi Wake, “Nimepewa mamlaka yote mbinguni na duniani.” Hakika. Huyu yuko nyuma yetu. Ati nini? Kwa kila ahadi aliyotoa, kwa sababu amepewa mamlaka yote, Baba amempa Mwana mamlaka yote. “Na kila kitu kilicho Mbinguni, kila mamlaka Mbinguni, ni Yangu,” alisema Yesu, “nami niko pamoja nanyi.” Kitu cha kutuunga mkono.

⁷⁷ Tukikumbuka jambo hili tunapoondoka, kuna Kitu fulani—kuna Kitu fulani nyuma yetu, Kitu fulani ndani yetu, na Kitu fulani mbele zetu. Amina. Hiyo ni kusema, “Njoo, amini, na uende.” Kitu fulani nyuma yetu, Kitu fulani ndani yetu, na Kitu fulani kikitutangulia. Alikuwapo, Yuko, na atakuja. Yesu yeye yule aliyekuwako, ni Yesu yeye yule usiku wa leo, na Yesu yeye

yule atakayekuja; yeye yule jana, leo, na hata milele. “Njoo, amini, na uende, na kumwambia mtu mwingine juu yake.” Amina. Loo, ninapenda hilo. Utukufu kwa Mungu!

⁷⁸ Uhai Wake, kile alichokuwa kwetu, ni maisha Yake ya huko nyuma, alitupa kile alichu ili kwamba tusidanganyike katika kile alichu leo. Loo, napenda hilo. Amina. Usichukue neno la mtu yeyote kwa ajili yake, chukua Neno la Mungu kwa ajili yake. Biblia ilisema, Yesu alisema, “Mkikaa ndani Yangu, na Neno Langu likae ndani yenu, mnaweza kuomba mtakalo, nanyi mtapewa.” Yesu alisema, “Ninii. . . Yeye aniaminiye Mimi, kazi nizifanyazo Mimi, yeye naye atazifanya.” Yesu alisema, “Bado kitambo kidogo na ulimwengu hautaniona tena, bali ninyi mtaniona, kwa kuwa nitakuwa pamoja nanyi, hata ndani yenu, hata ukamilifu wa dahari. Yesu Kristo yeye yule jana, leo, na hata milele.”

Tunajuaje? Watu wanasema, “Mbona hakika, ninaamini hilo.”

⁷⁹ Yesu alisema, “Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio.” Ishara hizo haziko juu yenu, kasema, “Huenda zikawa, labda zitakuwa, zinapaswa kuwa,” Yeye alisema, “*Zitakuwa.*” Vema. “*Zitafuatana* na hao waaminio.” Naam, bwana.

⁸⁰ Naye aliacha nini? Aliacha maisha Yake ya nyuma apate kutuonyesha kile alichokuwa. Hilo ndilo lililo nyuma yetu, ili tuweze kujua kitakachokuwa ndani yetu. Loo, sininii. . . Whiu! Tunaangalia nyuma kuona kile alichokuwa, ndipo tunaweza kuona sasa, kile alichu. Yesu kamwe hakuwa mwanatheolojia mwenye shingo ngumu, aliwaita kundi la wanafiki, na nyoka nyasini, na kadhalika, kuta zilizopakwa chokaa, makaburi yaliyojaa mifupa ya wafu; aliwakemea. Yeye hakujiunga na lolote la makundi yao, bali alidumu na Ujumbe kutoka kwa Baba. Alidumu na Maandiko, “Je, haikuandikwa katika Maandiko yenu?” Haidhuru walitaka kuona nini, na kile walichotaka kufanya, walitaka Yeye amfufue *huyu* na kufanya *lile*, Yeye akasema, “Ninafanya yale Baba anayonyesha kufanya. Sifanyi neno kwa nafsi Yangu, ila lile nimwonalo Baba akilitenda kwanza.”

⁸¹ Musa alisema Yeye angekuwa ni Nabii, Masihi alikuwa hivyo, Naye angeyatambua mawazo ya moyo wao. Naye Yesu alikuwa ni Neno la Mungu lililodhihirishwa, “Hapo mwanzo kulikuwako Neno, naye Neno alikuwako kwa Mungu, naye Neno alikuwa Mungu. Naye Neno alifanyika mwili, akakaa kwetu.” Yeye alikuwa ni Mungu katika mwili, na hiyo ndiyo sababu Neno la Mungu lilikuwa ndani ya Kristo, Naye alikuwa ni Neno la Mungu, nayo Biblia ilisema, ya kwamba Neno la Mungu, katika Waebrania mlango wa 4, ni kali kuliko upanga ukatao kuwili. Utafanyaje hilo na uwe mfuasi wa madhehebu fulani, useme,

“Hebu sema hivyo nasi tutakufukuza”? Utafanyaje hilo? Mwenye mashaka. Loo, jamani!

⁸² Na—najua ninajipatia adui, bali ninajifanyia marafiki Kule, kwa hiyo hilo ndilo jambo muhimu. Mnaona, sijali yale mwanadamu asemayo, ni yale Mungu asemayo. Niambieni si Neno. Angalieni mahali tulipofikia, jiangalie mwenyewe uone jinsi tunavyokufa. Inuka na ujitikise, rudi kwenye tukio la Pasaka la ufufuo ambapo Yesu Kristo anaishi leo. Yu hai sasa hata milele. Naam. Si . . .

⁸³ Ni yeye yule leo. Yeye alitutokea jana na kuthibitisha kile alichokuwa nyuma yetu, apate kuwa Kile kilicho ndani yetu. Na wa—wazo la kibadala niani mwetu la jinsi atakavyokuwa: Kama ni jambo tukufu jinsi hii anaposhuka miongoni mwetu sasa, itakuwaje tutakapokuwa na mwili kama Wake? Ndipo tunaona tuna kitu Fulani huko nyuma, kinachotutangulia, kimeenda mbele yetu kutuandalia mahali. Mungu ashukuriwe kwamba haitatubidi sikuzote kuwa viumbe vilivyofungwa ardhini!

⁸⁴ Ameondoka, Yeye ni . . . Alikuwa, tunaona kile alichokuwa, tunaangalia nyuma na kuona kile alichokuwa, kwa hiyo tunaona kile alicholeo. Kama Yeye alikuwa ni Mpambanuzi wa mawazo ya mioyo katika siku hiyo, wakati alipokuwa Neno, kama Yeye yuko hapa leo, Yeye ni Mpambanuzi yeye yule wa mawazo ya moyo. Kile alichokuwa, ndicho alicholeo, na atakuwa milele. Kama alikuwa ni Mwokozi mwenye upendo huko nyuma, Muumba, Yeye ni Mwokozi yeye yule mwenye upendo, Muumba leo, Naye yuko nyuma yetu, ndani yetu, na mbele yetu. “Njoo, na uamini, na uende, na kumwambia mtu mwingine.”

⁸⁵ Hatuamini hilo, la sivyo tusingeketi wafu hivyo pamoja na *taratibu* zetu zote za dini, kuwainua na kuwaketisha chini, na ninii yetu yote. . . Jumapili asubuhi, mioyo yetu ingekuwa inawaka kwa Moto wa Kipentekoste, tusingeweza kuvumilia hilo. Ilikuwa hivyo miaka arobaini iliyopita katika kanisa la Kipentekoste, bali mkaliundia dhehebu, mkaliua. Mliwaua—mliwaua wa—wa—mliwaua wale wanaotaka kuamini hilo, lakini kuna wengine ambao hawaamini hilo, wanaendelea kuishi.

⁸⁶ Wakati ile Nguzo ya Moto, mahali iliposimama, watoto walifanya kambi ndogo, kamwe hawakupiga hema zao kwa hali ya kudumu, kwa kuwa wakati wowote ile Nguzo ya Moto iliposonga, waliambatana Nayo. Luther aliiona na akatoka kwenye kanisa Katoliki. Lakini Luther alipokufa, walifanya nini? Waliliundia dhehebu, ile Nguzo ya Moto ikaondoka, naye Wesley akaifuata. Wesley alipokufa, waliliundia dhehebu, basi nini kilitukia? Nguzo ya Moto ikasonga mbele, nao Wapentekoste wakaifuata. Bila shaka, ubatizo wa Roho Mtakatifu. Sasa, Wapentekoste wameliundia dhehebu, nayo ile Nguzo ya Moto inafanya nini? Inasonga mbele, nao Wapentekoste wanakufa. Mbona, ni—ni kweli kabisa. Sio, tukio la Kipentekoste halifi, bali

madhehebu ya Kipentekoste hayafi, yamekufa. Lilifanya hivyo wakati lilipounda madhehebu.

⁸⁷ Wamekufa, kila mmoja. Mmoja hawezi—mmoja hawezi kuita . . . Birika haliwezi kusema chungu lina grisi, kwa sababu liko vivyo hivyo tu. Hiyo ni kweli. Wa Umoja hawawezi kuwakemea wa Uwili, nao wa Uwili hawawezi kuwakemea wa Utatu, nayo Assemblies haiwezi kulikemea Church of God, na Church of God haliwezi kulikemea United, wote wako kwenye kundi moja kubwa. Wakati walipounda madhehebu, walimwua, hawakumwua, walimfukuza kutoka miongoni mwao, kwa sababu walichora duara na, “Tuliingia *hapa*.” Mungu ni Mungu wa ulimwengu mzima, mwenye nguvu zote, aliye kila mahali, Yeye hafungwi na kanuni za imani za mtu yeyote. Amina. Kama Yeye yu hai, Yeye analithibitisha, kama halithibitishi, basi sivyo.

⁸⁸ “Njoo, amini, na uende, uone.” Naam, bwana. Shida yake ni kwamba, kwa ulimwengu, wanajaribu, kanisa linajaribu kuupa ulimwengu lundo kubwa la—la burudani. [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.] . . . ? . . . kwenye misingi yao, hatupaswi kufanya hivyo. Tunafanya nini? Tunawapa tu chungu kikubwa cha kitoweo cha kidini cha muligani kilichopikwa. Hivyo tu. Wanaziita karamu za kijamii, na michezo midogo ya karata, na supu ya jioni kumlipa mhubiri. Upuuzi! Hiyo si njia ya kuliendesha kanisa. Mungu alimtuma Roho Mtakatifu kuliongoza Kanisa. Sawa. Lakini tunajaribu kuupa ulimwengu . . . Mbona, huwezi kuwakabili hao watu na jambo hilo, tayari wanalo. Wao ni stadi sana katika burudani. Wana kipaji, kwa hivyo hatuwezi kuwafanyia chochote.

⁸⁹ Hebu na tuwape Kitu wasicho nacho. Haleluya! Kitu kimoja wasicho nacho ni Yesu. Amina. Usijaribu kujiburudisha pamoja nao, unakutana nao kwenye misingi yao. Mhubirini Kristo, na hebu waje kwenye misingi *huu*, ndipo mwone kile walicho nacho. Kama wanataka kukaa kwenye nchi ya vitunguu saumu, waacheni wakae. Hatupaswi kukutana nao kule, sisi si waigaji, sisi ni mitume. Haleluya! Hatuninii . . . Sisi si nyani, kama wasemavyo kuwa ndivyo tulivyo, sisi ni wana wa Mungu, walioumbwa kwa mfano Wake. Upuuzi kwa kundi hilo! Ondokeni kwake, kuna Kristo aliye hai. Amina.

⁹⁰ Loo, Kitu kimoja wasicho nacho ni Yesu. Loo, tu—tunaweza kuwapa yote . . . Loo, wana saikolojia nyingi sana, dini za kifalsafa, na kila kitu. Loo, loo, jamani, wa—wao—wao wamelemewa na hayo, bali kuna Kitu kimoja wasicho nacho ni Yesu. Hiyo ni kweli. Loo, wana burudani, wanaweza kufanya fujo kubwa zaidi ya mpira wa vikapu kuliko mnavyoweza, hakika wanaweza, wanaweza kuwaweka watu kwenye skrini hizo za sinema, huko nje, ambazo zingeweza kushinda chochote mnachoweza kufanya. Hiyo ni kweli. Wao ni hodari sana kwake, usijaribu kujilinganisha nao. Hivi Yesu hakusema wana wa ulimwengu, kile walicho? Hiyo ni kweli.

⁹¹ Lakini kuna Kitu kimoja wasicho nacho, ni Yesu. Na hilo ndilo tunalopaswa kuwakilisha, kuwaambia. Si kwamba tuna jumba kubwa la mazoezi ya viungo, na tuna darasa kubwa kuliko yote la shule ya Jumapili, na—na tunatoa *hiki*, na tuna chakula cha jioni, na tuna *hili* kwa ajili ya kanisa letu, na madansi, “Kama utakuja ujiunge na kanisa letu, tuna dansi kila Jumatano usiku. Kila Alhamisi usiku, baada ya mkutano wa maombi kwisha, tunacheza dansi kidogo kwenye orofa ya chini.”

⁹² Hapa hivi majuzi wakati hii, hivi mliiona picha hii kutoka London, iliyoingia kwenye skrini, ambapo yule kijana mpumbavu kule, kundi la, kanisa la Presbiteri, lilifanya mchezo wa kuigiza wa—wa kihuni wa ufufuo, ama, kusulubiwa? Ninayo papa hapa gazetini, nayo iliuisimua Uingereza kila mahali. Ilikuwa kwenye magazeti yetu hapa. Walikuwa na mvulana aliyevaa shati lenye milia ya peremende, na suruali ya jinzi iliyovutwa chini kwenye nyonga zake, naye ati alikuwa ni Yesu. Walikuwa na mwingine, Yuda, naye alikuwa akipiga gita ndogo namna *hii*, akitembea huku na huku, ikatangazwa kwenye televisheni kote nchini, “Nitamkamata usiku wa leo, mpenzi, nitamwuzi.” Na yote namna hiyo. Huku msichana mmoja akiyumbayumba-yumba na kuyumba-yumba, akisema, juu ya Yesu, akisema, “Nampenda mama yangu, maskini kipenzi, hilo si ni zuri vya kutosha, ewe mheshimiwa?” Namna hiyo. Wakitembea kote namna hiyo, wakati kanisa la kidini linaloinama chini hivyo, limekwisha! Watu walifanya nini? Walidhani ilikuwa ni nzuri sana.

⁹³ Vema, mnafikiri hilo ni jambo fulani? Moja kwa moja huko chini katika nchi yetu wenyewe, kila Alhamisi usiku katika kanisa fulani kubwa, la kimadhehebu, mchungaji, na hao wote, hufanya mchezo wa kihuni. Picha kwenye ukurasa wa mbele akiwa na ndevu ndefu, mhuni.

⁹⁴ Kanisa fulani la kimadhehebu, rafiki yangu alinipigia simu hivi majuzi usiku nishuke, wa dhehebu kuu la utakatifu, nao walikuwa wakifanya karamu ya kihuni, au, la, ya roki. Na hata yule mtu aliyekuwa akitangaza kwenye televisheni alisema, “Hivi huogopi kwamba utakosolewa?”

Akasema, “Kwa muda mrefu hii *ninii*, dhehebu hili la kanisa, limesahau ustadi mzuri wa roki.”

⁹⁵ Inapofikia mahali ambapo kanisa linalazimika kufanya burudani, ni kundi la watu wenye mashaka, waliorudi nyuma, wanaoelekea kuzimuni! Inapofikia mahali ambapo hatuwezi kumwakilisha Yesu Kristo katika nguvu za kufufuka Kwake, fungeni milango yenu na mrudi ulimwenguni, maana mmekufa kwa vyovyote vile. Amina. Naam, lakini ndivyo ilivyo. Um-hum. Loo, naam.

⁹⁶ Hatuwezi kumetameta kuwashinda. Yeye ni Nuru, Yeye ni Mmeko, si mng’ao. Yesu haninii, si mng’ao kama ulimwengu

unavyong'aa, bali Yeye ni mmeko laini wa Nuru. Amina. Wala huwezi *kuiangazia*, unapaswa kuiacha iangaze. Usijaribu kuichochea, kwa sababu haitafaulu. Hiyo ndiyo shida. Kama hawawezi kuwapata kwa njia moja, wanawapata kwa njia nyingine. Kama hawawezi kuifanikisha, kujaribu kuifanya nuru yao iangaze, wanafanya nini? Vema, wanajaribu... Hivyo ni vipodozi bandia. Huwezi kuifanya iangaze, acha tu iangaze. Loo, haleluya!

⁹⁷ Ni saa ngapi? Nilisikia kengele ya saa yangu, nami nimepita wakati. Amefufuka katika wafu, Yu hai. Ujumbe ni nini leo? “Njoo, amini, nenda ukawaambie wengine ya kwamba amefufuka katika wafu.” Yu hai, Naye anaonekana kwa Kanisa teule usiku wa leo. Kama alivyotokea wakati huo, kile anachofanya wakati huo, daima nimewaambia ya kwamba Mungu hana kikomo wala hawezi kubadilika, na kama huo ndio ulikuwa msimamo Wake kwa ulimwengu wakati huo baada ya kufufuka Kwake, ni jambo lile lile leo hii. Naye Yesu alishuhudia jambo lile lile kwa kusema, “Kama ilivyokuwa katika siku za Sodoma, ndivyo itakavyokuwa katika kuja kwake Mwana wa Adamu.”

Na tuinamishe vichwa vyetu.

⁹⁸ Bwana Yesu, wakati mwingine na—nashangaa kama sijarukwa na akili, ninapowazia juu ya kuona laana ya kutisha inayokuja juu ya ulimwengu huu, ninapowazia juu ya makanisa yanayotaribu kuwa waburudishaji, wakijaribu kuiga ulimwengu. Bwana Mungu, loo, Wewe—Wewe ulisema, “Baba, naomba ya kwamba uwaondoe ulimwenguni. Ondoa ulimwengu ndani yao, watenge na ulimwengu.” Uliomba kwamba wapate kulindwa, wanafunzi Wako, kutoka kwa ulimwengu, nao hawa hapa wakirudi moja kwa moja ulimwenguni, wakijaribu kujilinganisha na ulimwengu.

⁹⁹ Mungu, tujalie, tusaidie Bwana, mtu fulani ataushika Ujumbe, hakika, watajua. Wewe ni yeye yule jana, leo, na hata milele. Hujafa, bali u hai milele. Tunakuamini Wewe, Bwana. Basi mtu anawezaje kuamini usipomwita? Yesu alisema, “Hakuna mtu awezaye kuja Kwangu, asipoitwa na Baba Yangu kwanza. Na wote walioitwa na Baba Yangu, aliowaita, watakuja.” Nasi tunajua hiyo ni kweli. Watakuja. Na ni jukumu letu tu kuihubiri, na kuacha vibanzi vianguke popote vitakapo, nao kondoo waisikie Sauti.

¹⁰⁰ Mungu, hakika, baada ya kuzungumza juu Yako, juu ya kufufuka Kwako, taarifa kuu kuliko zote ya habari iliyopata kuenezwa ulimwenguni ni “Kristo alikufa kwa ajili yetu, naye amefufuka tena, anaishi ndani yetu, akitembea pamoja nasi, akiwa hai pamoja nasi, kujithibitisha Mwenyewe ndani yetu, yeye yule jana, leo, na hata milele.” Bwana, sijui jambo kuu zaidi.

¹⁰¹ Ninaomba sasa, ya kwamba waaminio wengi wataamini usiku wa leo, kwa kina zaidi, kwamba wasioamini wengi wataamini kwa mara yao ya kwanza, kwamba wengi ambao hawajajazwa na Roho Mtakatifu watajazwa na kuwa mtume Wako usiku wa leo, mwanafunzi mkuu atakayekufuata Wewe, na kwenda kuwaambia wengine. Jalia waiangalie Biblia na kuona ya kwamba Yeye alikufa, ili kwamba tuweze kuwa na majaliwa haya. Jalia waamini wanapomwona akitokea, na hebu basi waondoke kanisani, na waende wakawaambia wengine kwamba Yesu yu hai. Jalia waende kwa mioyo, na miguu myepesi na moyo mwepesi wakawaambie wengine, kama vile Theofilo na rafiki yake walivyofanya, wakitoka Emau.

¹⁰² Ee Bwana, hivi utaonekana mbele zetu usiku wa leo, hapa? Njoo miongoni mwetu na ufanye jambo fulani kwa . . .kwa ajili ya watu hawa, kama tu ulivyofanya kabla hujasulubiwa, wapate kujua ya kwamba Ujumbe wa wakati huu ni wa kweli, umefufuka katika wafu. Ninaomba, katika Jina la Yesu. Amina.

¹⁰³ Kweli ni wakati wa kufunga, lakini ninaamini, mwanangu alikutana nami pale mlangoni, na akasema aligawa kadi za maombi, naye mlinzi akaniambia, ama, yule mvulana ambaye hushughulikia taa, kwamba walikuwa wamegawa kadi za maombi wapate kuombewa. Ni wangapi, je, kuna yeyote humu ndani ambaye hajapata kuwa katika ibada zangu zozote hapo kabla ambazo nimemfanyia Bwana? Inueni mikono yenu, hujawahi kuwa katika mojawapo. Loo, vema, huenda tukafanya upambanuzi basi.

¹⁰⁴ Kama una . . .Kuna mtu yeyote hapa aliyekuwa katika . . . ambaye alikuwa . . .ambaye ninyi nyote mngekuwa, kwa kuwa ninatumaini mlikuwa Chicago hapa, mikutano mingi ambayo nimekuwa nayo . . .? Nilikuwa tu nikitaka kuomba ya kwamba Ndugu Tommy atakuja hapa na kusimama, tupate kuwaombea, kuzipitisha kadi, lakini kama hakuna mtu hapa ambaye amewahi . . .Ninaona theluthi mbili ya hili kusanyiko hawajawahi kuwa katika ibada nyingine.

¹⁰⁵ Kwa hiyo sasa, ninataka kusema hivi: Sidai kuwa mponyaji. Mtu yeyote anayedai kuwa mponyaji, yeye ni wa *kisigino*. Hiyo ni kweli. Sio m-p-o-n-y-a, hata hivyo. Mnaona? Lakini sisi—sisi . . .Kristo ndiye Mponyaji. Yesu tayari, pale Kalvari, amenunua wokovu wako na kununua ukombozi wako, Yeye alinunua uponyaji wako. Ni wangapi wanaojua hilo kuwa kweli? Jambo pekee analoweza kufanya ni kuonyesha Neno Lake, na kutimiza ahadi Yake. Hiyo ni kweli?

¹⁰⁶ Wakati alipokuwa hapa duniani, je, alidai kuwa ni Mponyaji? La, bwana. Yeye alisema, “Siwezi kufanya neno Mwenyewe, ila lile nimwonalo Baba Yangu akilitenda, ndilo atendalo Mwana vile vile,” Yohana Mtakatifu 5:19. Ni wangapi wanaojua hilo

kuwa ni kweli? Naam. Basi Yesu kamwe hakufanya lolote, mpaka alipoona ono.

¹⁰⁷ Mnakumbuka jinsi Yeye...? Vipi...? Ishara ya Masihi ilikuwa ni nini? Ni nani anayejua ishara ya Masihi ilikuwa iwe nini? Nabii. Hiyo ni kweli? Mpambanuzi wa mawazo na kutabiri. Wayahudi wote wanaamini ya kwamba Yeye alikuwa ni... Masihi anapaswa kuwa m—Mtabiri, Yeye ange—Yeye angejua yaliyokuwako, na yatakayokuwako, na yale yamekuwako, hiyo ilikuwa ndiyo ishara. Yote... Mungu alisema, “Akiwepo mtu miongoni mweni aliye wa kiroho, ama nabii, Mimi Bwana nitajitambulisha Mwenyewe kwake, nitasema naye katika ndoto na katika maono. Na kama yale asemayo yakitimia, basi mwogopeni nabii huyo, kwa kuwa niko pamoja naye. Lakini yasipotimia, basi msimsikie, msimwogope hata kidogo, maana siko pamoja naye.” Vema, hiyo ni akili tu.

¹⁰⁸ Na Wayahudi daima, watu wa Mungu waliochaguliwa, daima walikumbuka Mungu alinena nao kupitia kwa manabii. Waebrania 1 ilisema, “Mungu, alisema zamani na baba zetu kupitia manabii, katika siku hii ya mwisho kwa njia ya Mwanawe, Yesu Kristo,” sasa, katika nyakati hizi za mwisho, wasomaji wote wa Maandiko wanajua jambo hilo, katika Waebrania 1, Waebrania 1:1. Sasa, hebu tuanzia hapo mwanzo, “Mungu, alisema zamani na baba zetu kupitia manabii kwa njia mbalimbali, katika siku hizi za mwisho kwa njia ya Mwanawe, Kristo Yesu.”

¹⁰⁹ Sasa, Yeye alikuwa ni nani? Alikuwa Mfalme wa manabii, alikuwa ndiye mkuu kuliko manabii wote, kwa sababu Yeye alikuwa ndiye *yule* Nabii, “Bwana Mungu Wenu atawaondokeshea Nabii kama nilivyo mimi.” Ni wangapi wanaojua ya kwamba Musa alisema hilo katika...? Naam. Vema basi, Yeye alipokuja na kumwambia Petro jina lake lilikuwa ni nani, Simoni, na halafu, akanwambia jina lake lilikuwa Petro, alipomwambia Nathanaeli alimwona chini ya mti kabla hajaja, Nathanaeli alisema, “Hakika, Wewe ni Mwana wa Mungu; Wewe ndiwe Mfalme wa Israeli.”

¹¹⁰ Wakati alipomwambia yule mwanamke kisimani, kasema, “Nipe maji ninywe.”

Naye mwanamke akasema, “Mbona, Wewe Myahudi unaniomba mimi Msamaria? Tuna ubaguzi hapa, hatushirikiani.”

¹¹¹ Vema, Yeye alisema, “Lakini kama unajua ni Nani aliyekuwa akizungumza nawe, ungeniomba Mimi maji unywe. Nikupe maji usije kuteka, hapa kwenye kisima hiki.” Naye akaendeleza hayo mazungumzo. Alikuwa akifanya nini? Akiwasiliana na roho yake. Ndipo alipopata kujua shida yake ilikuwa nini... Ni wangapi wanaojua shida yake ilikuwa ni nini? Alikuwa na

waume wengi kupita kiasi. Kwa hiyo akamwambia, “Nenda, kamwite mumeo, mje naye hapa.”

“Loo,” akasema, “Si—sina mume.”

Akasema, “Umesema kweli, kwa kuwa umekuwa na waume watano, na yule unayeishi naye sasa siye mume wako, kwa hiyo umesema kweli.”

Sasa, mwangalieni mwanamke huyo, alijua zaidi juu ya Mungu kuliko nusu ya wahubiri wa Chicago. Hiyo ni kweli, hiyo ni kweli. Akasema, “Bwana . . .”

Sasa, angalieni yale hao wahubiri waliyosema walipomwona akifanya jambo hilo, walisema, “Yeye ni mpiga ramli, Beelzebuli.”

¹¹² Yesu akasema, “Ninawasamehe hilo, lakini siku moja Roho Mtakatifu anakuja kufanya jambo lile lile, nawe ukisema neno moja dhidi yake, halitasamehewa katika ulimwengu huu, wala ulimwengu ujao.” Hiyo ni kweli?

¹¹³ Mwanamke huyu akasema, “Bwana, naona ya kuwa Wewe ni nabii.” Kasema, “Tunajua, sisi Wasamaria, tunajua ya kwamba ajapo Masihi, Yeye atatwambia mambo haya.” Vema, hiyo ingekuwa ndiyo ishara ya Masihi.

¹¹⁴ Ikiwa Yeye ni yule yule jana, leo, na hata milele, hiyo ingali itakuwa ndiyo ishara ya Masihi. Hiyo ni kweli? “Kazi nizifanyazo Mimi, ninyi nanyi mtazifanya. Niko pamoja nanyi, hata ndani yenu, hata ukamilifu wa dahari.” Hiyo ni kweli, Ndugu Hicks? Mnaona?

“Tunajua Masihi yuaja, Naye atatuambia mambo haya, lakini u Nani Wewe?” Mnaona? “Huna budi kuwa nabii.”

Akasema, “Mimi ninayesema nawe, Ndiye.”

¹¹⁵ Na kwa jambo hilo akakimbia mjini na kuwaambia hao watu, akasema, “Njoni, mwone Mtu Ambaye ameniambia yale niliyofanya. Haimkini Huyu kuwa ndiye Masihi?” Nayu Biblia ilisema watu wa Samaria, kule, walimwamini Yesu kwa sababu ya ushuhuda wa huyo mwanamke. Hiyo ni kweli?

¹¹⁶ Sasa, Yeye alifanya ishara hiyo mbele ya Myahudi na mbele ya Msamaria, kwa sababu gani? Walikuwa wakimtaamia Masihi. Hiyo ni kweli? Hupati hata kisa kimoja mbele ya Mmataifa. La. Hilo . . . Mnaona, walikuwa wamefundishwa kwa maelfu ya miaka ya kwamba Masihi alikuwa yuaja, kwa hiyo Yeye alikuja . . .

¹¹⁷ Kuna jamii tatu tu za watu, hizo ni watu wa Hamu, Shemu, na Yafethi. Petro, akiwa na zile funguo, kwenye Siku ya Pentekoste aliufungua kwa Wayahudi. Filipino alishuka na kuwahubiria Wasamaria, akawabatiza katika Jina la Yesu Kristo, akawawekea mikono, Roho Mtakatifu hakuwa amekuja, Petro alikuwa na funguo, akashuka na kuwawekea mikono,

wakampokea Roho Mtakatifu. Huko juu, nyumba ya Kornelio, Petro alienda kule akiwa na zile funguo, akaufungua kwa akina nani? Wayahudi, Wasamaria, na Wamataifa. Na tangu wakati huo na kuendelea, Injili ikaendelea, kisha ikafunguliwa kwa watu wote: watu wa Hamu, Shemu, na Yafethi, sasa, kwa wale wana watatu wa Nuhu, ambao waliizaa jamii yote ya binadamu, kama tunaamini Biblia yetu, hao wengine waliagamizwa.

¹¹⁸ Hatuko huko nyuma katika nchi hiyo ya nyani, sisi, au, hao watu wa nyani, tunaamini sisi ni wanadamu, tumetoka kwa Mungu, tumefanywa katika mfano wa Mungu. Acha waamini wanayotaka kuamini, hili ndilo tunaloamini: Tunamwamini Yesu Kristo, Mwana wa Mungu, aliyefanywa kwa mfano wa Mungu, sio jambo la kushikamana na Mungu, alikuwa sawa na Mungu, na, “Mungu alikuwa ndani ya Kristo, akiupatanisha ulimwengu kwa nafsi Yake.” Yeye alikuwa Mungu, alionekana kama Mungu, alitenda kama Mungu, alihubiri kama Mungu, alifufuka katika wafu kama Mungu, Yeye ni Mungu. Hakika.

¹¹⁹ Ndipo tunamwona, wakati alipokuja na kusema, “Nitakuwa pamoja nanyi, hata ndani yenu. Kazi nizifanyazo Mimi, ninyi nanyi mtazifanya.” Sasa, Yeye aliahidi mwishoni mwa wakati wa Mataifa ya kwamba ishara hii ingeonekana. Sasa, hivi tunamtazamia Masihi? Hiyo ni kweli, tunakutazamia kuja kwa Bwana Yesu, yule Masihi. Vema, basi, Yeye aliahidi ya kwamba angeonekana.

¹²⁰ Sasa, kama Yeye aliwatokea kwa njia *hiyo*, hivyo vizazi viwili vya watu, kisha atuache tupitie tu kwenye theolojia, basi Yeye, huyo siye Bwana wetu Yesu. Loo, la, huh-uh, la. Mnaona, Yeye hana budi kutufanyia kama alivyowafanyia. Yeye anafanya nini? Kama alivyoahidi, katika siku za Nuhu na...?..., ninamaanisha, katika siku za Lutu, ndivyo atakavyokuwa sasa. Kwa hiyo Yeye amekuja kwa wateule Wake ambao wataliamini, na kujionyesha Mwenyewe ya kwamba Yeye angali ni Masihi, Yule aliyefufuka. Amina. Hiyo ndiyo Injili, ndugu yangu. Hakuna mtu anayeweza kuweka kidole kwenye hilo. Sasa, jambo ni kwamba, je, Mungu atatimiza Neno Lake? Ninaamini hilo.

¹²¹ Ni wangapi wenu walio na kadi za maombi? Inaonekana ni kama arobaini, ama hamsini. Vema, namba moja, ni nani aliye nayo? Kadi ya maombi namba moja, inua mkono wako. Ni herufu gani? Labda nina. . . Huh? A. A, namba moja, inua mkono wako, yeyote aliye na A, namba moja. Lazima umekosea, mahali fulani. Tutaanzia mahali pengine basi. Loo, samahani. Vema. Namba moja, njoo moja kwa moja hapa chini, mama.

¹²² Namba mbili, inua mkono wako. Vema, mama, njoo hapa. Namba tatu, inua mkono wako, namba tatu. Papa hapa, mama. Namba nne, namba tano. Papa hapa, mama, njoo hapa. Namba sita, namba saba, namba nane, nane, nane. Vema, tisa. Sikuona tisa. Tisa, kumi. Ni nani aliye na kumi? Kumi na moja, kumi na

mbili. Kusudi wote wasikurupuke mara moja. Kumi na mbili, kumi na tatu, kumi na tatu. Kadi ya maombi kumi na tatu. Waweza kuinua mkono wako? Kumi na nne, kumi na nne. Imekuwa polepole sana. Vema, vema, hebu . . . Hebu wasimame kwa dakika moja.

¹²³ Ni wangapi wasio na kadi ya maombi, inua mkono wako, nawe ni mgonjwa? Inua mkono wako. Sasa, si lazima uwe na kadi ya maombi. Niliwaomba mwamini hadithi hii ambayo nimesimulia kumhusu Yeye kuwa ni kweli.

¹²⁴ Kulikuwa na mwanamke katika Biblia, hebu tuseme yeye, alikuwa akitokwa na damu, tunaijua hadithi hiyo, hakuwa na kadi ya maombi, tuseme, pia, lakini akasema, “Ninaamini ya kwamba Mtu huyo ni wa Kweli, ninaamini Huyo ni Mwana wa Mungu, kama ninaweza kumgusa, nitapona.” Ni wangapi wanaijua hadithi hiyo? Na wakati alipomgusa, ilikuwaje? Aliondoka, labda, akaketi chini, kwa sababu aliridhika moyoni mwake kwamba alikuwa amemgusa Masihi. Mnaamini hilo?

¹²⁵ Sasa, sikilizeni, niangalieni, na mnisikilize. Mnaona? Alikuwa amemgusa Masihi, naye Yesu akageuka, akasema, “Ni nani aliyenigusa?” Sasa, wakati wakiwatayarisha watu hao. “Ni nani aliyenigusa?”

¹²⁶ Ndipo Petro akamkemea, akisema, “Vema, Bwana, kila mtu anakugusa. Kwa nini unasema, ‘Nani . . .?’” Kwa maneno mengine, “Ni kitu gani kinachokufanya useme jambo kama hilo? Mbona, watu watafikiri una kasoro. Mbona, unasema jambo kama hilo?”

Akasema, “Lakini naona kwamba nguvu zimenitoka.” Hiyo ni kweli?

¹²⁷ Vema, kama hilo lingemfanya Mwana wa Mungu ahisi nguvu zikimtoka, ingefanya nini kwangu mimi na kwako, mwenye dhambi aliyeokolewa kwa neema? Tusingeweza kufanya hivyo wakati mmoja, isipokuwa Yeye alisema, “Mambo nifanyayo Mimi, ninyi nanyi mtayafanya, na zaidi ya haya mtayafanya.” Ninajua King James inasema *makubwa zaidi*, lakini angalieni ile tafsiri halisi, *mengi zaidi*. Hakuna mtu angaliweza kufanya makubwa zaidi, maana Yeye alifanya kila kitu ambacho kingeweza kufanywa, mnaona, Yeye aliwafufua wafu, na kusimamisha maumbile, na kufanya kila kitu. Mnaona?

¹²⁸ Vema. Sasa, na maskini mwanamke huyo aligusa vazi Lake, Naye akahisi nguvu zikimtoka. Ndipo akaangalia kote kwenye kusanyiko, mpaka akaona mahali alipokuwa, naye akamwambia kuhusu kutokwa kwake na damu, na akasema imani yake ilikuwa imemwoko. Hiyo ni kweli? Hiyo ni . . .? Je, huyo alikuwa ni Yesu jana? Je, hivyo ndivyo alivyolifanya jana? Vema, kama Yeye ni yeye yule leo, si atafanya vivyo hivyo leo? Hakika, angefanya hivyo.

129 Sasa, ni yeye yule jana, leo, na hata milele. Je, hiyo ni kweli? Mnaamini hilo, Yeye amefufuka katika wafu? Basi ungewezaje kufanya...? “Vema, Ndugu Branham, ningemgusaje?” Sasa, ukitaka kumgusa afadhali usikilize yale ninayosema. Angalia, “Nitamgusaje?”

130 Yeye, sasa hivi, ni Kuhani Mkuu, Waebrania, mlango wa 3, kuhani Mkuu anayeweza kuguswa na mambo ya udhaifu wetu. Hiyo ni kweli? Sasa, mwili Wake umeketi Mbele za Mungu, kwenye kiti cha enzi cha Ukuu Wake. Hiyo ni kweli? Roho Wake yuko hapa Kanisani, Uhai Wake, ukiishi ndani yetu, na Yeye ni Mzabibu, sisi ni matawi. Mzabibu hauzai tunda, matawi huzaa matunda, mzabibu hutia nguvu matawi, Yohana 15. Hiyo ni kweli?

131 Sasa, kama Yeye ni Kuhani Mkuu yeye yule, nawe ungeweza kufikia Utukufuni na kumgusa kwa imani yako, Yeye angefanya nini? Kama Yeye ni Kuhani Mkuu yeye yule, angetenda vivyo hivyo, angefanya jambo lile lile. Ndipo utakapojitolea Kwake, nitajitolea Kwake, halafu kama ukigusa vazi La–Lake kwa udhaifu wako, ambalo Yeye aliahidi katika Biblia Yake ya kwamba atafanya, angalia kama atageuka na kutumia sauti yangu, na kuutumia mwili wako, kututumia sisi pamoja.

132 Ninyi huko nje kwenye kusanyiko, ambao hamtakuwa kwenye mstari wa maombi... Tutazifikia kadi hizi zote za maombi hivi karibuni, lakini hebu tuanze na ya–ya kwanza sasa, vema, sasa, kwanza, ninyi watu katika mstari huo wa maombi.

133 Ni wangapi huko nje ambao–ambao ni wagonjwa, ambao siwajui ninyi, inueni mikono yenu. Nyote huko nje mnaojua ya kwamba sijui lolote kuwahusu, inueni mikono yenu, kila mtu kwenye kusanyiko anayejua ya kwamba ninajua... .

134 Watu walio kwenye mstari wa maombi, ambao hatufahamiani kwenye huu mstari wa maombi, inueni mikono yenu, kwamba siwajui, inueni mikono yenu. Nafikiri ni asilimia mia moja, kote kote.

135 Vema, sasa, hii hapa picha nzuri... Mnakumbuka wakati nilipokuja Chicago kwa mara ya kwanza kuhusu jambo hilo, mimi... Kwa hiyo sasa, hii hapa pi–picha nzuri ya Biblia, hii hapa picha ya Yohana Mtakatifu mlango wa 4, huyu hapa mwanamke ambaye sijawahi kumwona, sijui lolote kumhusu, wala sijawahi kumwona hapo kabla maishani mwangu. Simfahamu. Hunifahamu, tunakutana kwa mara yetu ya kwanza.

136 Sasa, kama hili, katika ninii... Kuna mtu aliyewahi kuwa Palestina na kuona ambapo Yesu alikutana na mwanamke yule kwenye kisima kile? Ni mandhari, kitu kama hicho, huko nje, kisima kidogo huko nje ambapo Yeye alikuwa ameketi pale, akamwona huyo mwanamke. Sasa, huyu hapa mwanamume na mwanamke, wamesimama hapa, ambao hawajawahi kukutana

hapo awali maishani, nasi hatufahamiani. Nami naweza kuwaambia jambo hili kabla hatujaanza, yeye si wa taifa langu, kwa kweli haongei Kiingereza kizuri. Hiyo ni kweli. Huyu hapo Msamaria na Myahudi. Um-hum.

¹³⁷ Sasa, mimi si Yeye, bali Roho Wake Ndiye aliye ndani yangu. Na basi ikiwa Yeye ni yule yule jana, na hata milele, wala sijawahi kukuona, sijui lolote kukuhusu, wewe ni mwanamke tu anayekuja hapa, kama Mungu atanifunulia jambo fulani lililo maishani mwako, kama alivyomfanyia yule mwanamke pale, utajua kama ni kweli ama si kweli, u—ungejua, na halafu, kama jambo fulani ambalo umefanya, jambo ambalo limekuleta hapa, jambo linalokutatiza. Ama, kama sikujui, sijui lolote kukuhusu, kwa sababu. . . Unafanya ninii. . . una wakati mgumu, kwa namna fulani, kunielewa. Lakini kama sijui lolote kukuhusu, basi kama Yeye atalifunua, itabidi lipitie kwenye Roho mahali fulani. Unaamini hilo?

¹³⁸ Je, kusanyiko litaamini hilo? Sisi hapa, sote wawili pamoja. Sasa, Yeye yu hai? Basi, vipi kama mimi. . .? Kama alikuwa amesimama hapa, amevaa suti hii aliyonipa, sasa, kama mwanamke huyu angekuja, aseme, “Bwana, utaniponya?” unajua kile Yeye angesema? “Tayari nimefanya hivyo, umekombolewa.” Kama bidhaa imekombolewa kutoka kwenye duka la rehani, haiwezi kukombolewa mara ya pili. Tunayo risiti, hawawezi kututoza mara ya pili, tuna risiti. Nasi tuna risiti kutoka kwa Mungu. Amina. Gharama imelipwa, tumekombolewa, umeponywa.

¹³⁹ Kama nikimjia mwanamke huyu. . . Sasa, Yeye angefanya nini, akisimama hapa? Basi kama Yeye tayari amemponya. . . “Kwa kupigwa Kwake sisi *tuliponywa*.” Ililiweka wakati uliopita, *uliponywa*. Wahudumu wote, wasomaji wote wa Biblia wanajua hilo. Ni wakati uliopita.

¹⁴⁰ Sasa, kama Yeye—kama Yeye akija hapa, basi angefanya nini? Angeweza kujionyesha Mwenyewe yu hai. Nasi tungejuaje kwamba Yeye alikuwa hai? Kwa sababu Roho Wake angeingia ndani yetu, na kutenda vile vile tu alivyofanya alipokuwa hapa katika mwili Wake. Hiyo ni kweli? “Mimi,” kiwakilishi nafsi, “nitakuwa pamoja nanyi, hata ndani yenu. Kazi nizifanyazo Mimi, ninyi nanyi mtazifanya. Bado kitambo kidogo, na ulimwengu,” kosmosi, utaratibu wa ulimwengu, utaratibu wa kanisa, na kadhalika, “hautaniona tena, bali ninyi,” Kanisa, “mtaniona, kwa kuwa nitakuwa pamoja nanyi, nitakuwa hata ndani yenu hata ukamilifu wa dahari. Kazi nizifanyazo Mimi, ninyi nanyi mtazifanya.” Hii hapa. Je, Ujumbe wangu ni wa kweli? Kama ni wa kweli, basi Mungu atalitimiza Neno Lake.

¹⁴¹ Sasa, mama, niangalie kwa muda kidogo tu, ninataka kuzungumza nawe. Kufunga. . . Sababu ya mimi kukuleta hapa, ni kuninii, ili niweze kukutenganisha na watu wengine,

ili niweze kuzungumza nawe, kila mtu mwenye roho. Yesu aliwachukua, akawafukuza watu wote nyumbani hapo alipomponya binti ya Yairo. Alimchukua kiziwi, ama, kipofu na kumwongoza nje ya mji, mbali na umati, kusudi aweze, kumwondosha, apate kuongea naye. Hiyo ndiyo sababu nimekuleta hapa, kuna upako wa Roho.

¹⁴² Basi mwanamke huyo, huenda asinielewe, lakini kama unaweza kunielewa sasa, wewe kuwa mwaminifu kwangu. Sasa hivi tu jambo fulani lilikupata, hisia tamu sana, tulivu imekuja juu yako, sasa hivi. Kama hiyo ni kweli, inua mkono wako. Ninaangalia moja kwa moja ile Nuru mnayoiona kwenye picha, ambapo Yesu Kristo ndiye Nuru ile.

¹⁴³ Wakati alipokuwa hapa kwanza, alikuwa katika Mungu Baba, katika Nuru, wana wa Israeli waliifuata kupitia nyikani. Akasema, “Nimetoka kwa Mungu, nami naenda kwa Mungu.”

¹⁴⁴ Baada ya kifo Chake, kuzikwa, na kufufuka, Sauli alikuwa akienda zake Dameski, ndipo Nuru ikamwangusha chini, Nuru iyo hiyo, “Sauli, Sauli, mbona unaniudhi?”

Kasema, “U nani Wewe?”

Kasema, “Mimi ni Yesu.” Mnaona? Sasa, Hiyo ni Nuru ile ile.

¹⁴⁵ Sasa, kama Mungu atanielezea jambo fulani, wewe kuwa shahidi kama ni kweli ama si kweli. Uko hapa kusudi nikuombe kwa ajili ya ugonjwa wa wasiwasi unaougua, wasiwasi. Kama hiyo ni kweli, pungu mkono wako namna *hii*, ili watu waone. Sasa, kuna mambo mengine, una ugonjwa wa kibofu nyongo, ugonjwa wa kibofu nyongo. Na kwa kuwa ulisema hivyo wakati uo huo, Ndugu Hicks akisimama karibu, tutaona kama ni, ninii tu, kama ilikuwa ni kweli ama si kweli. Hebu na tuangalie tu kwa dakika moja zaidi. Naam, uko hapa kwa ajili ya mtu mwingine, mtoto wako mgonjwa, uliyemwacha nyumbani, mbali na hayo, una dada ambaye ana mtoto mgonjwa ambaye unamsimamia. Kama hiyo ni kweli, pungu mkono wako. Umepokea ulichoomba, imani yako imekuokoa. Nenda nyumbani, nawe utaikuta hivyo. Mungu awabariki. Kila kitu kitakuwa sawa sasa. Itakuwa yote. . . Mungu akubariki sasa, nenda ukiamini, kila kitu kitakuwa sawa kabisa.

¹⁴⁶ Unaamini hilo? Yeye yu hai? Sasa, unajua simjui mwanamke huyo. Ningewezaje. . .? Hata sijui nililosema, jambo pekee nitakalojua ni kuangalia kinasauti hiki, wakati kinapoyarekodi tena. Sasa, Biblia ilisema, “Kama wakisema, na likatimia, yale waliyosema, basi aminini.” Nimewaambia Yeye alifufuka katika wafu, Naye amelithibitisha, aminini. Amina.

¹⁴⁷ Sasa, hii hapa, hii hapa picha nyingine ya mwanamke mwingine, huyu ni mwanamke. Simjui huyu mwanamke, sijawahi kumwona, hatufahamiani. Nasi ni jamii mbili za watu, yeye ni, mimi ni Mwanglo-Sakson na—naye ni Mwethiopia. Sisi. . . Lakini walipozungumza na yule mwanamke kisimani,

yule Msamaria, wakati yule mwanamke Msamaria aliposema kulikuwa na ubaguzi, Yeye alimjulisha, upesi sana, ya kwamba hakuna tofauti kati ya rangi tulizokuwa nazo.

¹⁴⁸ Mungu ni Mungu wa jamii ya wanadamu. Nchi tulizoishi, na kubadilisha rangi zetu, hazina uhusiano wowote na kile tulicho. Mmoja alilelewa katika nchi moja ndipo akageuka manjano, na mwingine mweusi, na huyo mwingine kahawia, na huyo mwingine mweupe, na hilo halina uhusiano wowote, tunatoka kwenye mti mmoja, Adamu na Hawa. Hiyo ni kweli, jamii ya wanadamu ilitoka huko.

¹⁴⁹ Mungu wangu ni Mungu wenu, Muumba wangu ni Muumba wenu. Lakini wewe ni, ukiwa mwanamke mwe—mweusi, mimi, ninitwa mzungu, basi sisi ni jamii mbili mbalimbali za watu. Lakini tunasimama kama (ninajaribu kuwafanya waone jambo fulani.) Yohana Mtakatifu mlango wa 4, Yesu akikutana na mwa—mwanamke aliyekuwa Msamaria.

¹⁵⁰ Sasa, kama Mungu atanijulisha shida yako ni nini, utaniamini mimi kuwa ni nabii Wake, ama, mtumishi Wake? Sininii . . . Si—sina budi kuangalia neno hilo, ni jiwe la kujikwaa kwa watu wengi; kwa hiyo, tunajua na kuliamini, si lazima wajue. Unaugua vivimbe, vivimbe hivyo viko kwenye njia ya utumbo. Kama hiyo ni kweli, inua mkono wako. Kama Mungu ataniambia wewe ni nani, utaniamini? Alimwambia Simoni Petro kwamba yeye alikuwa ni nani, Yeye alimwambia. Hiyo ni kweli? Basi, Bibi Hall, nenda nyumbani, Yesu Kristo anakuponya. Amina.

¹⁵¹ Sasa, ninyi nyote watu weusi mwaminini Bwana, sasa hivi. Mnaona? Yeye ni Bwana Yesu, yeye yule jana, leo, na hata milele. Unamwamini Yeye? Iweni na kicho kabisa.

¹⁵² Vema hapa yupo, ninaamini dada mwingine mweusi. Njoo huku mbele. Hatufahamiani. Kama nilivyomwambia huyo mama, naamini ndivyo ilivyokuwa, huyo aliyepita, na hayo yote, mnajua wakati anaponiacha, katika ono, mimi, sijarukwa na akili, bali mimi . . .

¹⁵³ Unaingia kwenye ulimwengu mwingine, unaona mambo yaliyotukia zamani za kale, na jambo fulani likitukia mahali pengine, ndipo unashangaa umesimama wapi unaporudi, hiyo ndiyo sababu linanidhoofisha tu. Mnaweza kuona matokeo yake. Siku moja nitaondoka humu ulimwenguni, bali ulimwengu hautajua kamwe, mpaka tutakapokutana Huko, yale ninayopitia kujaribu kuwafanya wajue ya kwamba Bwana wangu ni halisi. Alifufuka katika wafu, Yeye hajafa, Yeye yu hai. Hmm! Nami ninaamini hilo kwa moyo wangu wote.

¹⁵⁴ Iwapo Mungu atanifunulia shida yako ni nini, kusudi isinilazimu kuingia katika mengi, kwamba tu shida yako ni nini, unaniamini mimi kuwa ni mtumishi Wake? Unaamini hadithi yangu kuwa ya kweli? [Huyo dada anasema, “Ndiyo.”—

Mh.] Vema. Wanasema unapaswa kufanyiwa upasuaji, ni kwa ajili ya uvimbe. Huo uvimbe uko tumboni. Hiyo ni kweli. Uliweka mkono wako juu ya tumbo lako, mtu fulani aliona hilo, nilihisi likitoka huko nje, kabla sijalisema. Sasa, iwapo Mungu atanifunulia jina lako ni nani basi, uta—utaniamini mimi kuwa ni nabii Wake, na mtumishi Wake? Bibi Cole, wewe rudi nyumbani, uwe mzima. Mungu akubariki, dada yangu. . . ? . . .

Mwamini Mungu, usiwe na shaka. Amini kwa moyo wako wote.

¹⁵⁵ U hali gani? Sasa, hawa hapa Mwanglo-Sakson na Mwanglo-Sakson. Hatufahamiani. Sikujui, lakini Mungu anakujua. Ikiwa Mungu atafunua. . .

¹⁵⁶ Sasa, hebu tu kidogo, kitu fulani kwenye kusanyiko, mtu fulani aligusa imani, mwanamke aliyeketi pale pale, huku ameinamisha kichwa chake akiomba, amevaa kofia ndogo ya kijani kibichi, ameketi papa hapa mbele yangu, mwanamke anayeonekana mkongwe, ameketi hapo, akiomba, akiwa na yabisi kavu. Vema, Dada, inua tu mkono wako. Uliangalia kote, na kuangalia kote, ukaangalia upande huo. Vema, yabisi kavu yako ilikuacha. Haikubidi kuja, kaa papo hapo ulipo. Nenda nyumbani, Yesu Kristo anakuponya.

¹⁵⁷ Ninataka kuwaulizeni ninyi watu jambo fulani, alimgusa Nani? Kamwe hakunigusa mimi, niko futi thelathini kutoka kwake. Lakini alimgusa huyo Kuhani Mkuu. Mnaamini?

¹⁵⁸ Sasa, yule mwanamke aliyeguswa, aliyemgusa Mungu, naye Mungu akamgusa, hatufahamiani, pungu mkono wako, mama. Hiyo ni kweli, sikujui. Mambo hayo yalikuwa ni kweli, yale yaliyosemwa. Hiyo ni kweli? Vema, umepata haja yako, ulimgusa Yesu Kristo.

¹⁵⁹ Huko hapa kwa ajili yako mwenyewe, uko hapa kwa ajili ya mtu mwingine. Mtu fulani anaingia upofu, wao ni vipofu, kipofu. Hiyo ni kweli. Hawako hapa. Ama wamekuwa California, au California, wako California, ni mwanamke. Unaamini? Basi nenda, na kama ulivyoamini, ndivyo itakavyokuwa. Usitie shaka. Mungu akubariki. Amini, usiwe na shaka.

Mnaamini huko nje, pamoja, ninyi nyote? Amini tu sasa, kwa moyo wako wote.

¹⁶⁰ U hali gani, mama? Vema. Ni tofauti kabisa, labda, katika umri wetu, labda. Lakini nijuvavyo mimi moyoni mwangu, hii ndiyo mara yangu ya kwanza kuwa pamoja nawe, kusimama karibu nawe. Sikujui, vivyo hivyo Mungu anakujua. Kama Mungu atanifunulia jambo fulani kukuhusu ambalo, kitu kama kilicho moyoni mwako, kitu unachotaka, ama—ama kitu fulani. . . nawe utajua kama ni kweli ama si kweli, wewe ndiwe mwamuzi wa hilo. Vema, kama Yeye anajua kile kilichokuwako, hakika unaweza kuamini Neno Lake kwa ajili ya. . . Kama

anaweza kukwambia yale yamekuwako, unajua kwamba yale yatakyokuwako, yatakuwa ni kweli. Vema, na alijalie.

¹⁶¹ Sasa, mahali fulani, Malaika wa Bwana aliondoka jukwaani. Roho wa Mungu alienda . . . Huyu hapa. Ni yule mtu mweusi aliyeketi hapa nyuma pembeni, akiomba. Unaugua mapindi. Kama hiyo ni kweli inua mkono wako. Vema. Uligusa Kitu fulani, Ndugu. Hukunigusa mimi, sikujui wewe, ulimgusa Kuhani Mkuu. Unamwamini Yeye? Basi imekwisha.

¹⁶² Mwamini tu Yeye, ninakuomba umwamini Yeye. Sijawahi kumwona mtu huyo maishani mwangu, kama nijuavyo, isipokuwa iwe ni mtaani, ama akipitia mahali fulani, ama kuja huku na huko katika kanisa hili, simjui huyu mtu. Kama wewe ni mgeni kwangu, bwana, inua mkono wako, ili watu waone jambo hilo, kwamba mimi na wewe hatufahamiani. Haya basi. Mnaona?

¹⁶³ Sasa, niambieni, ninataka kuwaulizeni: Mtu huyo aligusa nini? Yesu Kristo, Kuhani wetu Mkuu. Basi ujumbe wangu kumhusu Yeye ni kweli, Yeye yu hai. Basi aminini neno langu: Zikimbieni nyumba hizi za maiti, mkamwendee Kristo aliye hai, chukua jina lako, kama liko kwenye, kitabu fulani cha kanisa, sahu, weka jina lako katika Kitabu cha Mbinguni, kwa tukio jipya la kumkubali, na kuzaliwa mara ya pili.

Tuko wapi? Ni saa ngapi? Vema. Usiniache nikae muda mrefu sana.

¹⁶⁴ Sasa, ninaamini huyu ndiye yule mwanamke. Samahani, mama, i—i—inanibidi tu kuifuata Hiyo, jinsi inavyoenda, hivyo tu ndivyo ni—nijuavyo kufanya. Hebu na tumwangalie Bwana, tuone kile . . . Naam. Uko katika hali mbaya. Una uvimbe, nawe una wasiwasi juu yake. Unafikiri kama Mungu anaweza kuniambia huo uvimbe uko wapi, ingeisaidia imani yako? Ingeisadia? Uko kwenye titi, uko kwenye titi la kulia. Hiyo ni kweli, sivyo? Ngoja kidogo. Naam, una mtu fulani moyoni mwako, na ni mtu ambaye amekuwa Mkristo. Wewe ni, wewe ni mama wa msichana mraibu wa dawa za kulevya ambaye aliponywa matumizi ya dawa za kulevya katika mkutano wangu. Jina lake ni Helena, alikuwa mcheza dansi, ama *kitu kama hicho*. Naye msichana huyo anadhoofika, anamwacha Mungu, naye yuko moyoni mwako kumwombea, hiyo ni BWANA ASEMA HIVI. Hiyo ni kweli. Vema. Njoo hapa.

¹⁶⁵ Katika Jina la Yesu Kristo, mrudishe mtoto huyo, mponye mama huyu kwa ajili ya utukufu wa Mungu. Amina.

Usitie shaka, uwe sawa.

¹⁶⁶ “Kama unaweza kuamini, yote yanawezekana.” Unaamini? Ni wangapi wanaokumbuka kwamba hapo mwanzo, wakati ingenibidi kuushika mkono wa huyo mtu na kuuweka juu ya wangu, ungeona mambo hayo yakitendeka? Ni wangapi wanaokumbuka hilo? Ni wangapi wanaokumbuka ya

kwamba niliwaambia ya kwamba Bwana aliniambia itatimia, kama ningekuwa mnyenyekevu na mwaminifu, kwamba ningekuwa . . . ingefunua siri za mioyo, kama hawakuamini hiyo ishara ya kwanza, kama walivyoamini ya Musa, ishara ya pili ingetokea? Ni wangapi wanaokumbuka hilo? Mnasema, “Kwani Mungu huondoa karama?” La, bwana.

¹⁶⁷ Njoo hapa, bwana. Sikujui, hatufahamiani. Weka mkono wako juu ya wangu. Naam, bwana. Njoo huku juu. Ugonjwa wa tumbo. Hiyo ni kweli. Hebu niwaonyeshe jambo fulani. Angalia hapa, chukua huu mkono wako mwingine, weka mkono huu juu ya wangu. Hakuna tofauti, sivyo? Angalia *huu*, angalia hapa, hakuna tofauti. Sasa, ninaweka mkono wangu. Hakuna tofauti, sivyo? Sasa, angalia unapouweka mkono *huu*, tofauti inakuja, unavimba, na vitone vidogo vyekundu vinaupitia, ama, ninamaanisha vitone vidogo vyeupe vikiupitia. Angalia jinsi mkono wangu ulivyogeuka. Unaona? Hiyo ni kama nini. . . Angalia, jambo ni kwamba, kutiwa mafuta, hiyo ndiyo sababu ya kuweka mikono juu ya wagonjwa, chini ya upako, mnaona, kuweka mikono juu ya wagonjwa, iliyotiwa mafuta.

¹⁶⁸ Si mimi ninayefanya mambo haya, siwajui, siwajui hao watu, sikujui wewe. Lakini unaona, kuna kitu fulani ndani yako ambacho kingekuua. Unaona? Na hicho ni ibilisi, roho, *kitu fulani* hai, kinachokula, uhai unaojaribu kuondoa maisha yako, hiyo ndiyo sababu unarudisha mtetemeko tena.

¹⁶⁹ Sasa, angalieni tu, basi hakikisheni mnaangalia. Sasa, angalia hapa, si jinsi ninavyosogeza mkono wangu, bila shaka hivyo—hivyo vitu vyeupe . . . Angalia, unauona mkono wangu hapa? Unaona? Sasa, angalia, nitauchukua huu mkono wako, unaona, ninachukua mkono wako wa kushoto. Sasa, haifanyi hivyo hapo. Sasa, weka *huu* hapa. Sasa, haya basi. Unaona? Sasa, wewe ni mwanadamu tu katika mkono *huu* kadiri ulivyo katika mkono *huu*. Hiyo ni kweli? Lakini mnaona, ni kitu gani? Ni mkono wako wa kuume kwangu, kwamba unaniamini; ndio mkono wangu wa kushoto kwako, kwa moyo wangu, kwamba ninakupenda; mkono wangu wa kuume kwa Mungu, kwamba Yeye ni—Yeye ni Kiongozi wangu, Mwokozi wangu.

¹⁷⁰ Sasa, njoni hapa kwa dakika moja tu, nawatakeni mwangalie, hebu niweke mkono wangu *hapa*, mpate kuliona. Sasa, kama ukiondoka . . . Sasa, kwa Roho wa Mungu, ninaamini ninaweza kuufanya uondoke, bali siwezi kuuzuia, lakini kama unaweza kuuona ukienda, basi hiyo itakusaidia, sivyo, ku . . . ? Naam, bwana. Sasa, sasa, angalieni sasa, ili upate kuwa na hakika sasa, weka mkono huu *hapa*, ule nimeuwekelea mkono wangu. Unaona? Sasa, mkono huu mwingine *hapa*, unaona, ili wewe . . . Huo hapo. Sasa, ninawatakeni mfungue macho yenu, nawatakeni mtazame.

Ninalitaka kusanyiko kuinamisha vichwa vyenu, kwa dakika moja tu.

171 Baba yetu wa Mbinguni, si kuonyesha, bali tuko katika siku za mwisho, tuko katika saa za mwisho za siku, jua linatua, nuru za jioni zinaangaza, nabii alisema, “Itakuwa nuru wakati wa jioni.” Kasema kutakuwako na siku ambayo haitaitwa mchana wala usiku, hayo ndiyo tumekuwa nayo, madhehebu tu, madhehebu, bali wakati wa jioni, itakuwa Nuru. Nuru huchomoza mashariki na kutua magharibi, ustaarabu umesafiri pamoja na jua. Nuru ilizuka mashariki, juu ya watu wa mashariki, Mwana wa Mungu. Na sasa jua linatua magharibi, nao ustaarabu umehamia kote magharibi, kinachofuata ni mashariki, Nuru za jioni zinaangaza.

172 Huyu mtu anauangalia mkono wangu. Sasa, anaona hayo yangali yanatetemeka mkononi mwangu. Yeye ni mgonjwa, Baba, ninaomba kwa ajili ya rehema, ninaomba ya kwamba utafanya huo umwache, kwa njia ya Kristo Bwana wetu.

173 Sasa, ni mkaidi. Kabla sijafungua macho yangu, haujabadilika, vile vile tu. Hiyo ni kweli, bwana? [Ndugu huyo anasema, “Hiyo ni kweli.”—Mh.] Ni kitu kile kile tu. Sasa, hebu kidogo, kila mtu aamini sasa.

174 Bwana, nimeliambia kundi hili dogo la watu, hapa usiku wa leo, ya kwamba Wewe ulifufuka katika wafu, na kusema, “Kwa Jina Langu watatoa pepo.” Mtu huyo anajua ya kwamba ibilisi ni mtesi. Nalo neno *ibilisi* linamaanisha “mtesi.” Kwa hiyo anauangalia mkono wangu, anaona matendo yake kwa macho yake mwenyewe, anauangalia, yeye anaangalia aone kitakachotukia. Saidia, Bwana, Wewe ulitoa hiyo ahadi, ninakuamini Wewe.

Shetani, katika Jina la Yesu Kristo toka ndani ya mtu huyu!

Sasa, kabla sijausogeza mkono wangu, ama wewe kufanya lolote, umeondoka, sivyo? [Ndugu huyo anasema, “Naam.”—Mh.]

Sasa, fungueni macho yenu. Kamwe sikuangalia mkono wangu, naam, huo hapo.

175 Sasa, angalia hapa, bwana. Chukua mkono huu hapa. Unaona jinsi unavyoonekana? Chukua mkono huu hapa. Unaona jinsi unavyoonekana? Sasa, jambo fulani lilitukia, sivyo? Umetoweka, wewe uko huru. Nenda, Yesu Kristo alikuponya, amini kwa ninii yote . . .

176 Vema, unaamini kwa moyo wako wote? Mwamini tu Mungu, usiwe na shaka. Njoo, hebu mtu anayefuata aje. Sasa, usiwe na shaka, mwamini Mungu. Ningali ninahisi hilo huko nyuma, ya kwamba mimi . . . Sasa, angalieni, nitageuza kichwa changu, angalieni hapa.

177 Njoo hapa, mama, gusa tu mkono wangu. Kama Mungu atanifunulia, nikiangalia *huku*, shida yako ni nini, uniamini

mimi kuwa ni mtumishi Wake? Utafanya hivyo, huyu mama? Vema. Unaamini Mungu ataponya ugonjwa wako wa moyo, na kukupa afya? Unaamini? Atakufanya. . . ugonjwa wa moyo, akupe afya? Unalikubali? Inua mkono wako. Vema, nenda zako, uponywe, useme, “Mungu ashukuriwe.” Amini kwa moyo wako wote. Vema, bwana.

¹⁷⁸ Sasa, mama, kama utaamini ya kwamba kamwe hutalemazwa na yabisi kavu, Yeye atakuponya. Unaamini hilo? Endelea tu kusonga mbele, na kusema, “Asante, Bwana.” Nenda, amini. Vema.

¹⁷⁹ Njoo sasa, mama. Sasa, wewe ni mwanamke kijana. Shida yako ni wasiwasi. Kamwe huwezi kupata mahali pa kuanzia. Hiyo ni kweli? Kila- . . . wanakwambia, “Jirudie,” na yote yako akilini mwako, bali sivyo. Kitu fulani kinakufanya uogope, unaona, hiyo ni kweli, na kuogopa. Hapa ndipo mahali pako.

Toka ndani ya mwanamke huyu, Shetani! Ninakusahi, katika Jina la Yesu Kristo, kumwacha mwanamke huyu!

Sasa, umeanza, endelea tu mbele. Uponywe, katika Jina la Yesu Kristo.

¹⁸⁰ Njoo. Sasa, mwanamke huyu aliponywa wakati alipokuwa ameketi kitini, kitu kile kile, kwa hiyo afadhali uendele mbele tu. Wako ni wakati. . . Endelea tu kusonga mbele, Yesu Kristo anakuponya.

Unaamini kwa moyo wako wote? Hebu kidogo tu.

¹⁸¹ Huyu mama, kwa namna fulani ni mnene, aliyeketi pale akiniangalia, aliye na ngiri, unaamini ya kwamba Mungu atakuponya? Vema, unaweza kupata kile unachoomba.

¹⁸² Simjui huyo mama, sijawahi kumwona maishani mwangu, lakini alikuwa akiombea hili. Dakika chache tu zilizopita Nuru hiyo ilikuwa juu yake, alikuwa akiomba Mungu amwite usiku wa leo.

¹⁸³ Kama hiyo ni kweli, punga mkono wako huku na huku, mama, namna *hii*, unaona, ili wapate kuona. Vema, haya basi. Kama utaamini, utakuacha. Mwamini tu Mungu, usiwe na shaka. Amina.

¹⁸⁴ Huyu—huyo mwanamume anayefuata, la, ni mwanamke, karibu naye, aliyeketi hapo, akiugua maumivu hayo ya kichwa, unaamini ya kwamba Mungu atakuponya? Inua mikono yako ukipenda, ukubali uponyaji wako.

Mwamini Mungu, usiwe na shaka.

Vipi kama ningekwambia, tayari ulikuwa umeponywa, ungeniamini? Endelea tu kusonga mbele, Yesu Kristo anakuponya.

Hivi hamwoni Yeye ni Mungu?

¹⁸⁵ Hapa ameketi mwanamke mweusi, mwanamke wa pili ameketi pale kitini, ameketi pale pale, akiniangalia. Unaamini ya kwamba Mungu anaweza kukuondolea ugonjwa huo wa upungufu wa damu, na kukupa afya? Basi unaweza kupata kile unachoomba. Nenda, na uamini. Uh-huh. Uwe na imani.


Vipi kama ningesema, “Yesu Kristo anakuponya,” ungeniamini? Vema, nenda, ukaponywe.

¹⁸⁶ Vipi kama ningekwambia ugonjwa wako wa mgongo uliponywa ulipokuwa umeketi pale, unaniamini? Basi endelea tu kusonga mbele, ukisema, “Asante, Bwana.”

¹⁸⁷ Vipi kama ningekwambia wewe uliyeketi hapo chini, mama, “Amini kwa moyo wako wote, ugonjwa huo wa kichwa...” uliyevaa hiyo kofia nyeusi, huyo mama mweusi aliyeketi hapo hapo karibu, unaamini ya kwamba Mungu angeuponya huo, na kukupa afya, huo ugonjwa wa kichwa? Unaamini? Unaukubali? Inua mkono wako kama unaamini. Vema, unaweza kupata kile ulichoomba.

¹⁸⁸ Ni wangapi wenu huko nje wanaomwamini Bwana Yesu Kristo, wanaoamini ya kwamba Yeye ni Yesu aliyefufuka? Ni wangapi wanaojua ya kwamba “Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio”? Inueni mikono yenu. Ni waaminio wangapi waliopo hapa? Inueni mikono yenu. Ni wangapi wanaojua ya kwamba Yeye yu hai? Basi wekeaneni mikono nyinyi kwa nyinyi, nitawaombea, kila mmoja wenu anaweza kuponywa. Yeye hutimiza Neno Lake *hapa*, Yeye hutimiza Neno Lake *hapo*. Mnaamini hilo? Wekeaneni mikono nyinyi kwa nyinyi basi, na kuombeana.

¹⁸⁹ Baba yetu wa Mbinguni, tunalikabidhi kusanyiko hili Kwako, kama watu wanaoamini, Kristo aliyefufuka. Pasipo uvuli wa shaka, Wewe hujafa, bali u hai milele, yule Mshindi mkuu. Wamekuja, wameona, sasa jalia waende wakawaambie wengine ya kwamba Yeye hajafa, Yeye hayuko kaburini, ama kwenye dhehebu, bali Yeye yu hai katika mioyo ya watu Wake. Tujalie, kupitia Jina la Yesu Kristo.

Ndugu Hicks, chukua maikrofoni hii. 

61-0424 Taarifa Ya Habari
Iliyo Kuu Sana Katika Historia
Stephen Mather High School
Chicago, Illinois Marekani

SWAHILI

©2024 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS

P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.

www.branham.org